**DIOCESE DE KASONGO**
**SOEURS MISSIONNAIRES DE LA CROIX ET DE LA MISERICORDE ‘’ SMCM’’**
**Une famille religieuse au service des pauvres dans les périphéries**

# UWE MJUMBE WA MSALABA NA REHEMA YA MUNGU



Kitabu Cha Walaiki Wa Msalaba na Rehema ya Mungu

# UTANGULIZI

Walaiki wa Misionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu ni wanani ? Walaiki wa Misionari wa Msalaba na Huruma ya Mungu ni mkristu wowote aliyebatizwa ndani ya Eklezya Katolika, hasiye kuwa mtawa, na anayeishi duniani akisharikia maisha ya kiroho ya Jamaa ya Mabikira wa Wamisiori wa Msalaba na Rehema ya Mungu.

Walaiki wanaishi ndani ya jamaa yao, katika kijiji chao na nafasi yao ya kazi maisha ya kiroho ya shirika ya Jamaa iyo ya kitawa, yaani ***Kumtumainia Mungu na Kutenda matendo ya Huruma kwa jirani.***

Kwa ukomo huo, Wandugu « *wanakusanyika wakifanya fikara ya Neno la Mungu, kupokea sakramenta hasa sakramenta ya Kitubio na ya Ukaristia, wanasali kwa ajili ya wongofu ya wenyi zambi na kwa ajili ya roho za matoharani. Wanakusanyika vile vile kwa kutenda matendo ya Huruma.*

*Zaidi ya hayo, maisha ya kiroho na ya sala ya Walaiki wa Misionari wa Msalaba na Rehema italishwa na :*

- *Saa ya Huruma kuu ya Mungu ama saa ya Golgota*
- *Kutizama /Kuabudu- Msalaba*
- *Kufanya Njia ya Msalaba*
- *Kuabudu Ukaristia Takatifu*
- *Kusali kwa ajili ya Roho za matoarani*
- *Kusali Shapule ya Huruma ya Mungu na shapule ya Mama Maria*
- *Kusherehe sikukuu ya Rehema ya Mungu* » (Const. n°62).

Kitabu hiki ni msaada kwa maisha ya kiroho kwa ndugu Walaiki wa Misionairi wa Msalaba na Rehema ya Mungu. Kama vile tunasoma katika kanuni ya Jamaa letu la wamisionari : « tunapotizama Msalaba tunasikia moyoni mwetu maneno haya ya nabii Isaya : 'Nimekuweka kuwa mwangaza wa mataifa, ili wokovu wangu uenee mpaka miisho ya dunia' (Isaya 49, 6a). Juu ya Msalaba, Yesu anatusii na anatumainia ukarimu wetu ili tuendeleshe kazi ya ukombozi aliotimiliza kwa njia ya Mateso na kufa kwake Msalabani. Tunatumwa mpaka miisho ya dunia kutangaza yale tunayotizama juu ya Msalaba » (Const. n°4§1), yaani Mapendo makubwa ya Mungu na Huruma yake.

Ukomo wa kitume chetu ni « kumpelekea Yesu mioyo na kuunda Jamaa ya wandugu waliyookolewa na Kristu juu ya Msalaba » (Const. n°5). Kwa hiyo, « Tunakimbilia maombezi ya Mama Bikira Maria, Mama wa Rehema, yeye aliye simama wima chini ya Msalaba na kupokea utume wake. Mama wa Eklezya na Mama wa ndugu wote wa Yesu, anatufundisha kupokea, kama yeye, waana wote wa Mungu wanaotangatanga katika usiku wa zambi, wa umaskini na wa kifo. Kwa mfano wa Mama Maria, Mama wa Matumaini, tunaalikwa kuwa pahali pote alama ya matumaini tukileta uzima mpya, uzima tuliotolewa na Kristu juu ya Msalaba » (Const. n° 9).

Ndio maana, kwa njia ya sala tutatazama Msalaba, tutaabudu Msalaba, ili Yesu atufumbuliye yeye mwenyewe siri ya Huruma yake na atufanye kuwa wajumbe wa yale tutakayo tizama na

kuabudu chini ya Msalaba. Hivyo tutageuka kuwa wajumbe wa Rehema ya Mungu. Kama vile Mtakatifu Faustina anavyofasiria utume wa walaiki : « hawatafanya naziri yoyote, ila watajitolea katika sala na kutenda matendo ya huruma kwa ajili ya jirani. Kwa njia hiyo, watapokea neema na fazila nyingi. Ni watu wanaishi duniani. Wanao mapashwa ya kutenda kila siku tendo moja ya huruma kwa ajili ya jirani » (PJ1155-1158).

Kupitia fumbo la umwilisho wa Bwana wetu Yesu Kristu, na kwa namna ya pekee, mateso na kufa kwake Msalabani, tutafumbua zaidi ukumbwa wa Mapendo ya Mungu kwa ajili yetu. Juu ya Msalaba anatualika na kutusii tusharikie kazi ya ukombozi tukimpelekea mioyo « Naona kiu » (Yn 19, 28). **Msalaba na Rehema** ndio sura ya maisha ya kiroho ya Jamaa ya Wamisionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu. Msalaba ni alama kubwa na kamili ya Mapendo na Rehema ya Mungu. Alituonyesha Mapendo yake mpaka kufa na kufa Msalabani. Bwana Yesu juu ya Msalaba anatualika « *tuwe mwangaza », maana yake tupokee Mapendo hayo ya Msalaba na tuishuhudiye tukitenda matendo ya Huruma kwa ajili ya jirani.*

Basi, tukisaidwa na njia mbalimbali ya kupata Rehema ya Mungu kama vile Bwana Yesu Kristu alivyomfumbulia Mtakatifu Faustina, tutamwomba ***atugeuze kuwa Rehema*** ili wokovu wake ufike mpaka mipaka ya dunia tukitumia njia hizi tatu : ya kwanza - Kitendo cha Huruma haizuru aina gani ; ya pili - Neno la Huruma : nisipoweza kusaidiya katika matendo, nitasaidia kwa njia ya maneno ; ya tatu - Nisipoweza kushuhudia Huruma wala kwa matendo, wala kwa maneno nitaweza kuifanya kwa sala. Natuma sala zangu hata popote ninapozuiwa kufikia kimwili. (PJ 163).

.

## MSALABA NI ALAMA KUBWA YA MAPENDO NA HURUMA YA MUNGU

**Saa ya Huruma kuu ya Mungu ama saa ya Golgota (PJ 1320, 1572).**

Bwana Yesu alimwambia Faustina Mtakatifu : « Saa kenda inapotimia, omba Huruma yangu hasa kwa ajili ya wenye zambi. Nawe, haizuru hata kwa dakika chache tu ujizamishe mwenyewe katika mateso yangu, na kwa namna ya pekee katika moyo wangu uliojiachilia mkononi mwa Baba wakati wa kufa kwangu. Hivi, unaposikia saa kenda inagonga, ujizamishe kabisa mwenyewe katika Huruma Yangu ukiiabudu na kuitukuza : uombe uwezo wake kuu kwa ajili ya dunia nzima, hasa kwa ajili ya wenye zambi, maana ni wakati huo Huruma yangu ilifunguliwa kwa kila mtu. Saa ile unaweza kupata chochote unachoomba kwa ajili yako mwenyewe na kwa ajili ya wengine, saa hiyo ndipo neema inashinda Haki.

Binti yangu, ujikaze kufanya **Njia ya Msalaba katika saa hiyo**; usipoweza kufanya Njia ya Msalaba, ingia kanisani kwa dakika chache na kushangilia Moyo Wangu Mtakatifu unaojaa Huruma katika Sakramenta Takatifu ; na usipoweza kuingia kanisani, basi ujizamishe katika sala mahali popote ulipo hata kwa kitambo kidogo ».

Kiisha alimfumbulia sala ifuatayo ya kusali saa kenda mchana : **« Kifo chako, ee Yesu, ni asili ya uzima kwa ajili ya roho zote na ni bahari ya Huruma iliyomwagika kwa ajili ya Ulimwengu mzima. Ee kilindi hai chenye kujaa Huruma Takatifu, uukumbatie ulimwengu mzima na uujaze uzima wako kwa ajili yetu.**

**Ee damu na maji vilivyotiririka kutoka Moyo wako Mtakatifu kama chemchem ya Huruma kwa ajili yetu, ninakuaminia** ».

## NJIA YA MSALABA

**Sala ya kwanza**

Bwana Yesu, Mkombozi wa watu, ulifuata njia ya Msalaba katika mateso mengi siku ulipokufa msalabani. Twataka nasi kufuata njia yako.

Tunajua sasa kama ni zambi za watu na zambi zetu zilizokutiya katika mateso haya. Twajua vile vile kama ulikufa juu ya msalaba kwa mapendo ya watu. Twatubu zambi zetu zote, tukitaka kugeuza mwendo wetu. Tufanyizie tukumbuke vema mateso na mapendo yako, tutubu kabisa makosa yetu yenye kukutesa vile.

Ee Mungu, kwa mateso na kwa kufa kwake Mwana wako Yesu Kristu, uwape marehemu wanaoteswa Matoharani, rehema ya madeni yao, wapate kuingia katika furaha ya mbinguni. **Amen**.

***Wimbo wa mwanzo***

***Kituo cha kwanza*: YESU ANAHUKUMIWA AFE**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

1. **Somo la Biblia**

Pilato aliwaambia kundi la watu: ‘’Je, mwataka niwafungulie Mfalme wa Wayaudi?’’ Maana alitambua ya kuwa Wakuu wa makohani wamemtoa kwa wivu. Hao lakini wakachochea kundi la watu, waombe awafungulie zaidi Baraba. Pilato akasema tena, akawauliza: ‘’Basi mnataka nimfanyeje huyu, mnayemwita mfalme wa Wayaudi?’’ Nao wakalia tena: ‘’Msulubishe’’. Pilato akawaambia: ‘’Basi amefanya uovu gani?’’ Wakazidi kulia: ‘’Msulubishe’’. Naye Pilato, akitaka kuwatuliza kundi la watu, akawafungulia Baraba, akaamuru Yesu apigwe mijeledi, akamtoa ili asulubiwe (**Mk 15, 9-15**).

2. **Mafasirio**:

Mwana wa Mungu akakamatwa na watu wabaya, akafungwa, akapigwa, akatiwa miiba kichwani. Nyuma yake akakubali kuhukumiwa afe, tupate sisi uzima. Si Pilato peke yake aliyemhukumu Yesu, lakini sisi sote tulio hapa, pia wakosefu wa dunia yote, tumetaka wote kifo cha Mwokozi tulipokubali kukosa. Tumwambie basi kama tunatubu sana tukisema: Ee Yesu mwema, toba kwa zambi zetu tulizofanya.

3. **Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, wewe hukutenda zambi, lakini ulizuunguka popote ukiwatendea watu mema: na japo hiyo watu wa taifa lako walikutupa na kukusulubisha, na kuomba mtu mwovu afunguliwe. Tunkuomba utufanyizie tukumbuke sikuzote mema yako, tusikutupe tena kwa kutenda zambi, lakini tuwe waaminifu kwako mpaka kufa. Unayeishi na kutawala, milele na milele. Amen.

**V. Bwana utuhurumie**

**R. Bwana utuhurumie**

**V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.**

**R. Amen.**

Wimbo

### *Kituo cha pili*: YESU ANAPOKEA MSALABA

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

1**. Somo la Biblia**

Akibeba msalaba wake yeye mwenyewe, Yesu akatoka mji, kwenda mahali panapoitwa ***Fupa la Kichwa***, kwa Kiebrania ***Golgota*** (**Yn 19, 17**).

Kweli yeye amechukuwa mateso yetu, amejitwika huzuni zetu. Nasi tulimzania ameazibiwa, amepigwa na Mungu, ameshushwa. Sisi sote tulikuwa tunatangatanga kama kondoo, kila mmoja akifuata njia yake mwenyewe. Naye Bwana amemwangushia yeye maovu yetu sisi sote (**Yes 53, 4.6**).

2. **Mafasirio**:

Tuangalie namna gani Bwana Yesu anapokea msalaba huu mzito na upole wote, juu ya mabega yake yenye vidonda. Si Bwana Yesu anayestahili ule msalaba, lakini ingalitupasa kuubeba sisi wenyewe, sisi tulio na zambi. Tukiona Yesu akiubeba msalaba, anatufundisha tubebe msalaba wetu kwa upole, ndio mateso na uchungu wowote.

Kweli, Yesu mwema, si wewe uliyestahili kubeba msalaba, kwa sababu hukukosa, lakini sisi wakosefu tulitaka kukutesa kwa maovu yetu. Utufundishe kukufuata pasipo kunungunika, tukivumilia vema mateso yote na mashaka yote ya maisha yetu, kwa malipizi ya makosa yetu.

**3.Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, ulisema: ‘’Hakuna mtu anayenitwalia uzima wangu, ila mimi nautoa kwa kutaka kwangu mwenyewe’’. Kwa mapendo hayo makuu ulipokea msalaba wako, na kuuchukua mpaka Golgota. Tunakuomba: ututilie nguvu ya kuchukua magumu na mateso yetu bila kunungunilka, na kufuata mfano wako, uliyetaka kuteswa kwa ajili yetu. Unayeishi na kutawala, milele na milele. **Amen**.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

## *Kituo cha tatu*: **YESU ANAANGUKA CHINI YA MSALABA**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

1. **Somo la Biblia**

Yeye ameumizwa kwa ajili ya zambi zetu, amepondwa kwa ajili ya maovu yetu. Azabu inayotuletea amani ilimpata, na kwa vidonda vyake sisi tumepona (**Yes, 53, 5**).

**2. Mafasirio**:

Yesu ameendelea katika njia ya Kalvario, akiregea sana. Msalaba ulikuwa mzito mno. Anashindwa na uzito wake, hata anaanguka chini. Na mimi, nilikwaa na nilianguka mara ngapi, nilipotenda zambi? Uzito wa msalaba wa Yesu ni zambi zetu sisi.

Ee Yesu wangu mwema, utufanyizie tusiongeze uzito wa msalaba wako, kwa kutenda zambi tena.

**Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, uliona msalaba wako ni mzito, hata ukaanguka chini yake; lakini ulisimama tena na kujitwika msalaba wako kwa nguvu ya mapendo yako. Tunakuomba: utuhurumie sisi tunaposhikwa na magumu mazito, ututilie nguvu ya kuyavumilia kwa mapendo, tupate kuungana nawe katika kazi ya kuwakombowa watu. Unayeishi na kutawala, milele na milele. **Amen**.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

### *Kituo cha nne*: YESU ANAKUTANA NA MAMAE

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

**1. Somo la Biblia**

Simeoni alimwambia Maria: ‘’mtoto huyu amewekwa aangushe na kuwasimamisha watu wengi katika Israeli, awe alama inayoleta ubishi, kusudi yaonekane wazi mawazo ya mioyo mingi. Nawe mwenyewe, upanga utachoma moyo wako’’ (Lk 2, 34-35).

**Mafasirio**:

Nani awezaye kupima uchungu wa Yesu na Maria, wote wawili walipokutana katika njia ya msalaba? Bwana Yesu alimwona mama yake mpenzi, akilia kwa uchungu na hakuweza kumtuliza. Bikira Maria alimwona Mwana wake mtakatifu, akiteswa sana hakuweza kumsaidia.

Ee Mama Maria mtakatifu, Mama wa Yesu na Mama mwenye kuteswa naye, utupatie sisi sikitiko la kweli kwa zambi zetu, tusikubali kukosa tena. Tulilie zambi zetu siku zote za maisha yetu.

**2. Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, katika njia yako ya msalaba, upanga wa uchungu ulichoma moyo wa Mama yako, alipokuona wewe, mtoto wake, umevikwa taji la miiba na kuchukua msalaba wako. Tunakuomba: uwatulize mama wanaoona uchungu sababu ya watoto wao wagonjwa, utusaidie na sisi tuwe na moyo wa kusharikia mateso yako na ya mama yako. Unayeishi na kutawala, milele na milele. Amen.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

*Kituo cha tano*: **SIMONI ANAMSAIDIA YESU KUCHUKUA MSALABA WAKE**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

1. **Somo la Biblia**

‘’Mtu akitaka kuwa mfuasi wangu, ajikatae mwenyewe, ajitwike msalaba wake, tena anifwate. Kwani mtu anayetaka kuokoa uzima wake, ataupoteza; lakini mwenye kupoteza uzima wake kwa ajili yangu, yeye atauokoa. Yamfaa nini mtu kuupata ulimwengu wote, akijipoteza mwenyewe, au kujitia hasara? Kwani mtu anayeona haya juu yangu na juu ya maneno yangu, juu ya mtu huyu Mwana wa Mtu ataona haya, atakapokuja katika utukufu wake’’ (**Lk9, 23-26**).

**Mafasirio**:

Heri kwake Simoni, mtu wa Kirene aliyemsaidia Bwana Yesu kuubeba msalaba wake. Hivyo Bwana Yesu anatufundisha kama kila mtu duniani anapashwa kuuchukua msalaba pamoja naye, na kuyaunga mateso yake na mateso ya Mkombozi wa watu. Anatufundisha vile vile tuwahurumie watu wengine, tukiona mateso yao. Mkristu wa kweli asikumbuke wala asitolee mateso yake tu, lakini anawahurumia wote wenye kuteswa. Tena anafanya nguvu kwa kuutuliza uchungu wa watu wote.

Ee Yesu mwema, nikipata masumbuko au mateso, nataka kuyachukuwa kwa sababu yako, nikifuata mfano wa Simoni aliyepokelea msalaba wako. Unitilie moyo mkuu nisiyakatae, lakini niyapokee kwa kitubio.

**2. Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, ulitaka Simoni wa Kirene achukue msalaba wako nyuma yako, unatuita na sisi wafuasi wako tujitwike msalaba wetu kila siku na kusharikia mateso yako. Tunakuomba: kwa kuwa sisi watu zaifu hatuwezi kitu bila wewe, utupatie sikuzote msaada wa neema yako, ili tuwe hodari katika kushika mapenzi yako, na tukupendeze katika matendo yetu yote. Unayeishi na kutawala milele na milele. **Amen**.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

***Kituo cha sita*: MWANAMKE MTAKATIFU ANAPANGUZA USO WA YESU**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

1. **Somo la Biblia**

Hakuwa na uzuri, wala wangavu wa kuvuta macho yetu, wala hakuwa na umbo safi la kutupendeza. Alizarauliwa na kuachwa na watu: yeye mtu wa huzuni, alizoeya kuteswa; sawa na mtu mwenye kuepukwa na watu alizarauliwa, wala hatukumheshimu hata (ang. **Yes 53, 2-3**).

**Mafasirio**:

Veronika akamkuta Bwana Yesu katika mateso mengi sana. Uso wake umeenea jasho na damu. Akimwona vile, mapendo yake Veronika yameshinda woga wa askari. Akamkaribia Bwana Yesu na hodari, akampangusa uso wake kwa kitambaa.

Ee Yesu wangu, unapita uzuri waana wa watu wote, lakini kwa mapendo yetu sisi, umekuwa kama kidudu chenye kutupwa. Tunakuomba: utie mfano wa sura yako ndani yetu, tupate kufanana nawe katika vitu vyote. Ututilie moyo mkuu, tusiogope kufanya vema na tupate kuendelea kama wakristu wa kweli mbele ya watu.

**2. Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, ulisema: ‘’Yeyote mnayotendea mmojawapo katika hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi’’. Tunakuomba: vile kama mwanamke Yule alivyokuonyesha mapendo akipangusa uso wako, tukutumikie kwa mapendo katika watu wenzetu. Unayeishi na kutawala, milele na milele. Amen.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

***Kituo cha saba*: YESU ANAANGUKA MARA YA PILI**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

**1. Somo la Biblia**

Bila sababu wamenitegea wavu wao, bila sababu wamenichimbia shimo, wapoteze uzima wangu.

Nilipoanguka mimi, walifurai, wakakusanyika juu yangu wanipige mimi, nisipozani kitu. Wakanirarua bila kupumzika, wakanisumbua, wakanifanyizia mzaa, wakanisagia meno. Wakanifumbulia kinywa sana, wakisema: ‘’Weye, weye, tumeona kwa macho yetu’’ (**Zab 34, 7.15-16.21**).

**Mafasirio**:

Kwa kuanguka mara ya pili, Bwana Yesu anatuonyesha uzaifu wetu. Mara nyingi tunaangukaanguka, tukirudi kila mara katika zambi. Tukumbuke mateso gani Bwana Yesu ameona kwa zambi zetu za siku zote. Lakini kama vile Bwana Yesu anasimama pale pale, akiendelea katika njia yake ya mateso, hivyo sisi pia inatupasa kusimama pasipo kuregea, tukijua vema kama njia ya kwenda mbinguni inajaa na miiba. Furaha ya milele inapita katika njia ya mateso.

Ee Yesu, twakuomba sana neema na nguvu za kuacha zambi zetu zote, kwa kukufuata siku zote pasipo kuacha.

**2. Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, ukikubalia kuzarauliwa na kupigwa na kuchekwa na watu waovu; utupatie sisi nguvu ya kudumu imara tunaposumbuliwa na kutukanwa kwa ajili yako, tupate kuvumilia hayo kwa mapendo yako. Unayeishi na kutawala, milele na milele. Amen.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

*Kituo cha nane*: **YESU ANAWATULIZA WANAWAKE WANAOMLILIA**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

**1. Somo la Biblia**

Mkutano mkubwa wa watu walimfuata Yesu, na wanawake wenye kujipigapiga kifua na kumwomboleza. Yesu akageuka na kuwaelekea, akawaambia: ‘’Enyi mabinti wa Yerusalemu, msinililie mimi, ila mjililieni wenyewe na kuwalilia watoto wenu. Kwani siku zitakuja watakaposema: Heri walio tasa, na matumbo yasiyozaa, na maziwa yasionyonyesha. Hapo wataanza kuiambia milima: Tuangukieni; na vilima: Tufunikeni. Kwa sababu wakiutendea vile mti mbichi, yatakuwaje katika mti mkavu?’’ (**Lk 23, 27-31**).

**Mafasirio**

Bwana Yesu anaona machozi ya wanawake wale waliomlilia na anawatuliza katika uchungu wao. Lakini alipowatuliza akisema wasimlilie yeye, ila zaidi wawalilie watoto wao. Bwana Yesu anatuonyesha wazi wazi kama uchungu wetu si wa kweli tukisahau kwanza kulilia zambi iliyo kati yetu.

Ee Yesu wangu, unifundishe kuona na huruma mateso na uchungu wa watu wenzangu, nipate kuwasaidia na kuwatuliza. Najua kama tumestahili mateso na uchungu juu ya zambi zetu. Nasikitika sana makosa yangu yote.

**2. Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, si Wayaudi tu waliokutesa, ila na sisi pia, tuliozidisha mateso yako kwa zambi zetu. Tunakuomba: utupatie sisi roho ya kutubu, tuzililie zambi zetu na za watu wenzetu. Utuhurumie, ee Yesu, utuondolee makosa yetu. Utufanyizie tuvumilie magumu yetu kama malipo ya zambi za dunia. Unayeishi na kutawala, milele na milele, **Amen**.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

***Kituo cha kenda***: **YESU ANAANGUKA MARA YA TATU**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

**1. Somo la Biblia**

Alipotendewa vikali, yeye alinyenyekea, wala hakufunua kinywa: kama mwana kondoo anayenyamaza mbele ya mwenye kukata manyonya yake, hakufunua kinywa. Ameondoshwa, amefungwa, amehukumiwa: nani aliyeshurulika na mwisho wake? Amekatiliwa mbali na nchi ya wazima, amepigwa kwa ajili ya uovu wa taifa lake. (ang. Yes 53, 7-8).

**Mafasirio**:

Bwana Yesu anafika karibu ya Kalvaryo. Hawezi tena kwendela, mateso yake yalimshinda, na anaanguka mara ya tatu. Lakini anasimama, anaendelea katika njia yake ya mateso kwa kufika mahali pa kusulubiwa. Kwa kuanguka hivi mara tatu, Bwana Yesu alitaka kutufundisha tusiache kufanya nguvu kwa kuomba uhodari, kila mara tunapoanguka katika zambi.

Ee Yesu mwema, kwa uchungu wa kuanguka kwako mara tatu, unipe neema ya kurudi upesi kwako nikikukosea. Sitaki kufuata desturi ya watu wapotevu wenye kuzoea hali ya zambi, wakibakia siku nyingi, hata miaka mingi, pasipo kuondolewa.

**2. Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu wewe usiye na kosa, ulikubali kutendwa vikali na kuteswa na kupelekwa kuchinjwa kama kondoo, wala hukufunua kinywa. Tunakuomba: utufundishe sisi kufuata mfano wako, na kuvumilia magumu na matukano ya watu bila kunungunika, na kuacha kisasi tukitendwa vibaya, ili tushinde maovu kwa kutenda mema. Unayeishi na kutawala, milele na milele, **Amen**.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

***Kituo cha kumi:*** **YESU ANAVULIWA NGUO ZAKE**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

**1. Somo la Biblia**

Askari walitwaa nguo zake Yesu, wakafanya mafungo mane, kwa kila askari fungo moja. Wakatwaa kanzu yake pia. Ile kanzu haikuwa na mshono, ikawa yote mfumo mmoja tokea juu. Kwa hiyo wakaambiana: ‘’Tusiipasue, lakini tuipigie kura, itakuwa ya nani’’. Litimie Andiko lisemalo: ‘’Waligawa nguo zangu kati yao, wakaipigia kanzu yangu kura’’ (Yo 19, 23-24).

**Mafasirio**:

Tukumbuke mateso gani Bwana Yesu ameona, waaskari walipomwondosha nguo zake. Anatufundisha vile kama ni lazima kwetu tuache mazoezi mabaya, hata kama tunateswa kwa kuyaacha. Mara nyingi tunakosa nguvu kwa kurudi katika njia ya zambi. Saa ile tukumbuke namna gani Bwana Yesu ameteswa walipomwondosha nguo na kuongeza mateso ya vidonda vyake vyote.

Ee Yesu, kuanguka katika zambi ni kwepesi kwa sababu roho yetu ni zaifu, lakini kuamka na kuacha mazoezi mabaya ni kugumu sana kwetu. Utuletee mapendo na neema ya utakaso na ya roho safi.

**2. Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, ulipovuliwa nguo zako, vidonda vyote vya kupigwa mijeledi vilifunguliwa tena, nawe uliteswa vikali katika mwili wako wote, upate kulipa zambi za usherati. Tunakuomba: utupatie sisi nguvu ya kushinda tamaa mbaya, ili tuishi katika usafi wa mwili na moyo. Unayeishi na kutawala, milele na milele, **Amen**.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

*Kituo cha kumi na moja*: **YESU ANASULUBIWA**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

**1. Somo la Biblia**

Wakamsulubisha Yesu, wakakaa chini, wakamchunga pale. Juu ya kichwa chake wakaweka mshtaka wake, ulioandikwa: ‘’Huyu ni Yesu, Mfalme wa Wayaudi’’. Hapo wakasulubiwa pamoja naye wevi wawili, mmoja kuume, na mwingine kushoto. Nao waliopita njiani wakamtukana wakitikisa vichwa vyao, na kusema: ‘’Ewe unayebomowa hekalu na kulijenga tena kwa siku tatu, jiokoe mwenyewe, kama ndiwe Mwana wa Mungu, ukushushe msalabani’’. Nao Wakuu wa makoani na Wazee, wakisema: ‘’Ameokowa wengine, kujiokowa mwenyewe akashindwa’’ (Mt 27, 35-42).

**Mafasirio**:

Yesu anafungwa msalabani. Anajitolea yeye mwenyewe sadaka ya mapendo, kwa wokovu wa watu. Waaskari wanampigilia misumari katika mikono na miguu na wanamweka katikati ya wakosefu wawili. Roho yetu ielekee mlima wa Kalvaryo, kuangalia kazi kubwa ya ukombozi wetu. Tuangalie na machozi Mkombozi wetu mwenyewe kupita kipimo cha mtu yeyote wa dunia. Tusikie basi uovu wa zambi.

Ee Bwana Yesu, mateso na damu yako yasitupotee bure, Damu yako isafishe roho zetu ikatupatie nguvu kwa kuzilinda safi; mateso yako yatuwashie moyo, tukupende kuliko vitu vyote, siku zote za maisha yetu.

**2. Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu ulitimiza kabisa mapenzi ya Baba yako, na kuwatii watesaji wako waliokusulubisha, na kuvumilia mateso makali ya msalaba na matukano ya watu. Tunakuomba: utufundishe sisi kushika mapenzi ya Baba, na kupenda amri zake, na kuvumilia magumu ya maisha bila kunungunika. Unayeishi na kutawala, milele na milele, **Amen**.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

***Kituo cha kumi na mbili***: **YESU ANAKUFA MSALABANI**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

**1. Somo la Biblia**

Karibu na msalaba wa Yesu, walikuwa wakisimama mama yake, dada wa mama yake, Maria mke wa Klopa, na Maria Magdalena. Yesu alipomwona mama yake, na yule mfuasi aliyempendelea anasimama karibu yake, akamwambia mama yake: ''Ee mwanamke, huyu ndiye mwana wako''. Halafu akamwambia mfuasi: ''Huyu ndiye mama yako''. Na tangu saa ile, yule mfuasi akampokea kwake. Kiisha Yesu, akijua kama yote yamekwisha kutimia, ili Andiko litimie kabisa, akasema: ''Naona kiu''… Yesu alipokwisha kupokea siki, akasema: ''Yametimia''. Akainamisha kichwa, akatoa roho (Yn 19, 25-30).

(***Hapo ikiwezekana, watu hupiga magoti na kusali kwa ukimya muda mfupi***)

**Mafasirio:**

Hakuna siku kubwa kupita siku ile, Yesu Kristu, aliye Mwana wa Mungu, alipotimiza kazi yake yote kubwa ya kuwakombowa watu binadamu, Yesu anatoa roho: ''Yatimia''. Na tena akilia na mlio mkubwa, akasema:'' Baba, naweka roho yangu mikononi mwako''. Na kisha kusema vile, akainama kichwa, akazimia roho.

Ee Yesu wangu mwema, umekufa sababu ya zambi za watu. Umekufa kwa ajili ya kila mmoja wetu. Aksanti sana kwa mapendo yako makuu. Twakuomba utie moyoni mwetu mapendo yako, tupate kukupenda kupita vitu vyote wewe uliyeleta uzima wako kwa sisi wakosefu tusipotee milele.

**2. Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, ulitaka Mama Maria asharikie mateso yako, akisimama chini ya msalaba wako, na mbele ya kufa ulimtoa awe mama yetu sisi wote, ili ashurulike nasi kwa mapendo ya mama. Tunakuomba: utupatie sisi kusharikia mateso yako pamoja naye, na kwa msaada na maombezi yake tuongeze kazi yako ya ukombozi, tukifanya kazi ya kitume kati ya watu wenzetu. Unayeishi na kutawala, milele na milele, Amen.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

*Kituo cha kumi na tatu*: **YESU ANASHUSHWA MSALABANI**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwa sababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

**1. Somo la Biblia**

Kwa maana ilikuwa siku ya Matayarisho, Wayahudi walimwomba Pilato miguu yao waliosulubiwa ivunjwe, na miili iondolewe. Wakaja askari, wakamvunja yule wa kwanza miguu, tena yule wa pili aliyesulubiwa pamoja na Yesu. Lakini walipofika kwa Yesu, wakiona amekwisha kufa, hawakumvunja miguu, lakini mmoja wa askari alimchoma ubavu kwa mkuki: mara ikatoka damu na maji. Baada ya hayo, Yosefu wa Arimatea akamwomba Pilato ruusa ya kuondoa mwili ya Yesu. Pilato akampa ruhusa. Basi akaja, akaondoa mwili wa Yesu (ang.Yn 19, 31-38).

**Mafasirio**:

Bikira Maria anaupokea mwili wa Bwana Yesu mikononi mwake. Anaangalia uso wake uliochafuka kwa damu na ulioharibika kwa mateso makuu. Zamani uzuri wa uso wake ulipita uzuri wa binadamu wote. Sasa Maria mtakatifu anaona sura ya Mwana wake mpenzi inajaa na uchungu.

Ee Bikira Maria, hiyo ndiyo kazi ya zambi zetu. Tusaidie, tupate kutubu namna ya kweli makosa yetu, tusirudie tena katika udanganyifu wa shetani, lakini tufuate Mwana wako aliyetupenda na aliyekufa kwa kutukomboa.

**2. Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, moyo wa Mama Maria ulichomwa kwa upanga, alipomwona askari anakuchoma ubavu kwa mkuki, na kiisha alipokea mwili wako ulioumizwa vibaya. Tunakuomba: utufanyizie tusharikie moyoni uchungu na mateso ya mama yako, na pamoja naye tutimilize ndani yetu, yaliokosekana katika mateso yako, tukitolea taabu na magumu yetu kwa ajili ya wokovu wa dunia. Unayeishi na kutawala, milele na milele, **Amen**.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

***Kituo cha kumi na nne*: YESU ANAZIKWA KABURINI**

V. *Tunakuabudu, ee Yesu na tunakusifu*.

R. *Kwasababu umewakombowa watu kwa msalaba wako mtakatifu*

**1. Somo la Biblia**

Akaja pia Nikodemo, yule aliyemjia Yesu usiku kwanza, akaleta mchanganyo wa manemane na udi. Wakatwaa mwili wa Yesu, wakaufunga vitambaa, pamoja na yale manukato, kama ilivyo desturi ya kuzika watu kwao Wayaudi. Pale aliposulubiwa, palikuwa na bustani, na katika kaburi jipya, wala hata mtu hajatiwa humo bado. Humo basi wakamweka Yesu. (ang. Yn 19, 39-42).

**Mafasirio** :

Yosefu wa Arimatea, pamoja na watu wema wengine wanamweka Bwana Yesu kaburini. Katika mawazo ya watu ni mambo ya mwisho, lakini mbele ya macho ya Mungu si vile, kwa sababu kaburi ya Bwana Yesu si nafasi ya mauti, ila nafasi ya uzima. Sikukuu ya Paska, Bwana Yesu amefufuka, watu wote wapate kujua kama ndiye Mungu Mwana.

Yesu mwema, uliyefufuka kwa kututakasa, tunakuomba sana utuokoe sisi sote siku zote, zaidi, mateso yako yasiwe bure kwetu. Utupe nguvu kwa kukufuata katika magumu ya maisha yetu, tupate kusharikiana nawe, katika sifa ya uzima wa milele.

**2. Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, ulisema: ‘’Mbegu ya ngano inayoanguka katika udongo isipokufa, inakaa peke yake tu; lakini ikifa, inazaa matunda mengi’’. Tunakuomba: utufanyizie tuwe tayari kujitoa kabisa kwa ajili yako, na kukutumikia mpaka kufa katika watu wenzetu. Unayeishi na kutawala, milele na milele. **Amen**.

***V. Bwana utuhurumie***

***R. Bwana utuhurumie***

***V. Roho za marehemu, kwa rehema ya Mungu, zipumzike kwa amani.***

***R. Amen.***

Wimbo

**Kiisha njia ya Msalaba**

1. **Somo la Biblia**

Kama tumekufa pamoja na Kristu, twaamini ya kama tutaishi vile vile pamoja naye. Twajua hakika : Kristu, aliyefufuka katika wafu, hafi tena : mauti haina uwezo juu yake tena. Nanyi vile vile : mjiangalie kwamba mmekwisha kuifia zambi, na sasa mnaishi kwa ajili ya Mungu, katika Kristu Yesu (ang. Rm 6, 8-11).

**Sala** (*Kiisha muda mfupi wa ukimya*)

Ee Yesu, baraka yako ishuke kwa wingi juu yetu sisi tuliokumbuka mateso ya kufa kwako. Utuongezee imani na mapendo, utusabitishe katika kusudio letu la kukufuata katika njia ya msalaba, ili tuishi sikuzote kwa ajili ya Mungu, Baba yetu, tukikataa zambi na kushika mwendo safi, na pamoja nawe tufike mpaka utukufu wa ufufuko. Unayeishi na kutawala, milele na milele. **Amen**.

## KUABUDU MSALABA

1. **Wimbo**
2. **Ingilio Ukimya :** kujiweka mbele ya Mungu tukiomba msaada wa Roho Mtakatifu atuangazie, aje asali ndani mwetu.
   Tunautazama Msalaba alama ya Mapendo makubwa ya Mungu kwa ajili yetu. Mungu anayeteswa kwa ajili yangu, kwa ajili ya ulimwengu : « Alinipenda, akajitoa kwa ajili yangu » ili anikomboe.

3. **Sala ya mwanzo :**

   *Sala ya kusali mbele ya Msalaba*
   Ee Yesu mwema mno, ninakuangukia nikikuomba kwa kutaka sana, upende kutiya moyoni mwangu imani, matumaini na mapendo yako. Unifanyizie nitubu kweli zambi zangu, na nitake sana kugeuza mwendo wangu ; ndio hayo ninayo kuomba sana, nikiangalia kwa uchungu vidonda vyako vitano, ninakusikitikia sana moyoni mwangu na kukuonea huruma, nikikumbuka maneno hayo ya Daudi Nabii : « Wakanitobowa mikono na miguu, wakaniesabia mifupa yote » Amen.

4. **Neno la Mungu :** (linasindikizwa na fikara fupi)

5. **Kutazama Msalaba**
   - Hatua itatusaidia kutizama kwa imani na sala Msalaba Mtukufu wa Yesu (étapes pour la contemplation de la Croix glorieuse de Jésus). Si lazima kufuata maneno ya hatua zote. Hiyo ni mfano tu, ila ya lazima ni kusimama muda wa kutosho kwa yale Roho Mtakatifu anatuvuta nayo katika sala. Pengine ni neno la Mungu, pengine ni hali fulani ya maisha yetu inayoangaziwa na mateso yake Bwana

Yesu, pengine ni hali ya jamaa yetu hama ya dunia… Ya lazima tujitie mbele ya Yesu Msulubiwa tukimwomba Roho Mtakatifu asali ndani mwetu.

- Tunatazama Yesu Msalabani KATIKA UKIMYA.

Tunakumbuka mapendo yake makubwa. Tunautazama msalaba tukirudishia moyoni mwetu neno moja, tendo moja la Yesu Msulubiwa.Tunakumbuka maneno yake juu ya Msalaba :

*« Mungu wangu, Mungu wangu kwa nini umeniacha » ?« Leo utakua pamoja nami katika paradizo » ; « Baba uwasahe sababu hawajui watendalo » ; « Mwanamke, huyu ni mwana wako ; Yoane, huyu ni Mama yako » ; « Naona kiu » ; « Yametimia » ; « Baba mikononi mwako naiweka Roho yangu ».*

- Tunatazama mateso ya Moyo wake, vidonda vyake, matusi, upekee, kuzarauliwa, mapigo, kusulubiwa. Tunatazama Yesu anayetuangalia kwa macho ya huruma. Tunamtaza Yesu anayechukua mateso yetu yote. Watu wadogo, wamaskini, wagonjwa, wote wanaotupiliwa, wanaoteswa na njaa, na kiu, watu wanaokosewa haki, wafungwa, wakimbizi, watu wanao kosa amani. Tunakumbuka maneno haya : « chochote mtakao mtendea mmoja kati ya hawa wadogo, mnanitendea mimi ». Tunakumbuka wakosefu wasioamini hasa wale wanaokata matumaini ya kuokoka. Tunakumbuka wale tuliowakosea na wanaokosa amani sababu yetu.

  Tunaomba huruma kwani : « Yesu anateswa sababu sisi tunakataa kupokea mapendo yake ». Tunaomba huruma sababu kwa zambi zetu tunaongeza kumtesa tena leo Yesu Kristu. Tunaomba huruma kwa ajili ya ulimwengu mzima hasa kwa ajili ya wale wanaozarau mateso yake Yesu.

- Tunamshukuru kwa ajili ya mapendo makubwa na ya ajabu. « Amenipenda akajitoa kwa ajili yangu ». Tunajitolea kwa Yesu : Jibu langu kwa Mapendo ya ajabu ya yesu kwa ajili yangu. Ninajitolea kwake. Ninatolea maisha yangu kwa Yesu, jamaa zetu, nia yetu ya kumtumikia – Makusudio yangu ya kumpenda zaidi, ya kuwa mwaminifu kwake ; nitampelekea miyo ili nitulize kiu chake Yesu …

- Nunaomba msaada wa Mama Maria ili nitimize vema makusudio hayo.

## 6. Litania ya Msalaba Mtukufu wa Bwana Yesu

Bwana utuhurumie
Kristu utuhurumie
Bwana utuhurumie

Msalaba wa Yesu uniokowe
Msalaba wa Yesu mti yenye mwangaza unikoe
Msalaba wa Yesu alama ya mapendo uniokoe
Msalaba xa Yesu nguvu ya Mungu uniokoe

Msalaba wa Kristu unilinde
Msalaba wa Kristu zidi ya shetani unilinde
Msalaba wa Kristu zidi ya mahadui wa Eklezia unilinde
Msalaba wa Kristu zidi ya ubaya wote unilinde

Msalaba ya Mwana Kondoo unisafishe
Msalaba ya Mwana Kondoo msinji wa Imani yangu unisafishe
Msalaba ya Mwana Kondoo kwa magonjwa yangu unisafishe
Msalaba ya Mwana Kondoo kwa mateso yangu unisafishe

Msalaba wa Yesu zawadi ya maisha unitakase
Msalaba wa Yesu zawadi ya maisha inayoshinda maadui wangu unitakase
Msalaba wa Yesu zawadi ya maisha inayokaza nafsi yangu unitakase
Msalaba wa Yesu zawadi inayogeuza maisha yangu unitakase

Msalaba wa mapendo ya Utatu Mtakatifu uniokowe
Msalaba wa mapendo ya Utatu Mtakatifu maondoleo ya zambi uniokowe
Msalaba wa mapendo ya Utatu Mtakatifu wokovu wa Waamini uniokowe
Msalaba wa mapendo ya Utatu Mtakatifu moto wa mapendo uniokowe

Msalaba wa Yesu mpiganaji wa giza unikinge
Msalaba wa Yesu mpiganaji wa giza ya ukali unikinge
Msalaba wa Yesu mpiganaji wa giza ya ujanja wa shetani unikinge
Msalaba wa Yesu mpiganaji wa vita za roho za utchafu unikinge

Msalaba wa wokovu ubarikiwe
Msalaba wa wokovu msinji wa maisha ubarikiwe
Msalaba wa wokovu mwanga ulio juu ubarikiwe
Msalaba wa wokovu mlango wa amani ya milele ubarikiwe.

7. **Sala ya mwisho.**

- Kwa ajili ya Msalaba wako alama ya imani yetu na imani ya Babu zetu : *utupatie nguvu ee Yesu, ututakase*
- Kwa ajili ya Msalaba wako Mtukufu unaochukua Mwili wako na kupokea Damu yako : *ututakase ee Yesu na usafishe zambi zetu zote*
- Kwa ajili ya Msalaba wako uliopigiliwa misumari katika mikono na miguu : *ukubali kushuudia ndani mwetu na utubariki*
- Kwa ajili ya ungaro wa Msalaba wako Mtukufu : *fukuza giza na ubaya wote na utuangazie ee Yesu*
    - Msalaba Mtakatifu wa Yesu, *ninakuheshimu*
    - Msalaba Mtakatifu wa Yesu, *ninakutukuza*
    - Msalaba Mtakatifu wa Yesu, kwa ajili ya Moyo wa Mama Maria uliochomwa : *ukubali kutuponya na kutuokoa.* Amen

**WIMBO**

**MSAADA MWENGINE KWA KUTIZAMA NA KUSALI CHINI YA MSALABA :**

**KUTAZAMA MOYO MTAKATIFU WA YESU**

***Ee Yesu unayetobolewa misumari Msalabani***

Moyo wako unapasuka. Mapendo uliotaka kitupatia haikukubaliwa. Mapendo uliotaka kupokea haukuipewa sababu moyo wetu unaokosa shukrani. Moyo wako, moyo wa kimtu unaowaka na mapendo ya kimungu unavunjika.

Moyo wako unatupiliwa, unazarauliwa !!! Uso wako unatemewa mate, unajaa machafuko za kila namna. Unasulubiwa, unavikwa taji la miiba kichwani. Sasa unatundikwa msalabani. Wako wapi wale uliowapa moyo kwa maneno yako matulivu ? Wako wapi wale uliowaondoa katika utumwa wa shetani na kuwaponya magonjwa ya kila namna ? Wote wanakuacha !!! Rafiki yako Yuda anakutoa !!! Rafiki yako Petro anakukana !!! Hakuna hata mmoja aliekuwa tayari kwa kukesha pamoja nawe !!! Hata mmoja anasikia ukubwa wa Mapendo yako !!!

***Ninakutazama ee Bwana wangu***

Ninaona Moyo wako unaochomwa mkuki, ninaona nafasi hiyo Moyo wako unafunguliwa. Ninapoangalia, macho yangu inaona machungu ya Moyo wako. Moyo wako unavunjika ! Moyo wako ee Bwana unachukua mateso na mahangaiko ya ulimwengu mzima : machungu ya watoto walio achiliwa, jamaa inayokosa mapendo na kuvunjika, wagonjwa, wakimbizi wanaotanganga huku na huku kukosa nyumba ya kupumzikia, wanakosa maji, chakula, matunzo ; Moyo wako unachukua wafungwa wanaozulumiwa ; ninatazama katika Moyo wako ma elfu na ma elfu ya watu wanaokufa peke yao na wanaosahauliwa. Ninaona nyuso ya wengi wanaokosa matumaini, nyuso zao zinajaa uchungu, macho yao inahangaika kutafuta kitulizo.

Ninapotizama Moyo wako unaochomwa mkuki ninawaona wote wanaoteswa sababu ya kuachiliwa, kutupiliwa, kuzarauliwa. Ninawaona wote nafasi ile umechomwa mkuki. Moyo

wako unafunguliwa na ninatazama mateso ya ulimwengu mzima unayoyachukua na unasharikiana na kila binadamu.

Moyoni mwangu ninasikia sauti hii : « Njooni kwangu nyinyi mnaosumbuka na kuelemezwa na mizigo, mtapata kitulizo » (Mt 11, 26-30). Ninakuja kwako ee Bwana, nina jitupilia ndani ya Moyo wako. Unijalie nafasi ya pekee ili nionje ukubwa wa Mapendo yako kwangu.

(*Kulinda ukimya ili kila mmoja ajitolee katika Moyo Mtakatifu na mwenyi Huruma wa Bwana wetu Yesu Kristu*).

***Ee Yesu mwenyi Huruma***

Eee Yesu mwenyi Huruma sana, Moyo wako unavunjika sababu ya tunakataa kupokea Mapendo yako. Watu wa kale na sisi tungali hai hata wale watakaozaliwa wanapita chini ya Msalaba wako, wanaona mateso yako juu ya Msalaba lakini wengi hawatambui alama ya wakovu wao : « Watamwangalia yule waliomchoma » !!! Ni nani anayekutizama na mapendo ?

Unijalie ee Yesu Mwema sana, moyo wa imani nitambue hapo nafasi ya wakovu wangu na nikuabudu !!!

***Ee Yesu, Moyo wako unachomwa mkuki***

Ninaona maji na damu inayotoka katika Moyo wako unaochomwa mkuki. Yule aliyeona wa kwanza alitambua alama kama Wewe ndiye aliyeshuhudiwa na maandiko, alitupasha yale aliyoyaona ili nami pia nipate kusadiki kama Wewe ni yule mwenyi hata mfupa mmoja haikuvunjwa na nikuangalie kama « Yule aliyechomwa ».

Unishushiye Roho yako ee Bwana, nipate kukutazama kwa imani kama yule alichomwa ili aniokowe !!!

***Maji na Damu***

Maji na damu inatoka katika ubavu uliochomwa. Unisaidie kuelewa fumbo hilo ee Bwana. Damu mingi inamwagika tangu miaka, damu ya watu wasiojuwa sababu gani walikanyagwa, walichinjwa, walikosa maziko ya heshima, silaha za kila namna na mabombe zinaongeza kumwaga damu na kuharibu sura ya maelfu ya watu wanaume, wanawake kama vile watoto.

Damu hiyo inatiririka kutoka katika mioyo yenyi hasira, uwivu, tamaa ya kulipisha kisasi ; mioyo inayosukumwa na chuki, fitina, ukali, hamu ya kubomoa. Tangu damu ya Abeli aliyeuwawa na nduguye mpaka damu ya wote wanaouwawa bila sababu, damu hayo yote yanalia mbele ya Mungu.

Damu yako ya bei kubwa inatiririka kwa kuponya moyo wangu unaovunjika, moyo wa kuvunji wa kila baba, mama na watu wengi duniani kote.

***Ninatazama Moyo wako uliochomwa***

Ninaona damu inayotoka katika Moyo wako. Moyo wako usiojua chuki wala kisasi, wala wivu, wala fitina… bali Huruma, Shukrani, Mapendo, Amani, shuruli ya kutuliza na kupana moyo. Ubaya hauna na nafasi katika Moyo wako, ila Mapendo tu.

Damu inayotiririka kutoka Moyo wako ni Damu ya Mwana Kondoo asiye na kosa, anayeondoa zambi za dunia. Wewe ee Bwana ni Sadaka kamilifu ; unaotaka kutuingiza pamoja nawe mbele ya Baba yako wa mbinguni.

***Nitazama Moyo wako***

Ninatazama moyo wako na ninaona siyo tu damu ila pia maji. Kama vile damu, maji pia inaweza kua kiini cha kubomoa. Kama vile tufani kuu wakati wa Noe, vile vile huku na huku maji inabomoa nafasi nyingi.

Lakini, ***maji inayotoka katika ubavu wako unaleta uzima***. Inanitakasa na zambi na inaniingiza katika dunia mpya, mahali mapya na jamaa mpya. Ni maji inayotoka katika mwamba kwa kukata kiu cha waana wa israeli. Ni maji ya Yordani yenyi waana wa israeli walivuka pamoja na sanduku la Agano wakiingia katika inchi ya Agano. Ndani ya maji hiyo ulibatizwa na Yoane Mbatizaji. Ni maji iliyo geuka kuwa divai pa arusi ya Kana. Ni maji ya miujiza ya kisima cha Betsaida. Ni maji yenyi ulinawisha mitume wako miguu.

Ndio ee Bwana, maji inayotoka katika Moyo wako ni hayo yote na zaidi ya hayo kwa njia ya maji haya unatupatia uzima wako na unatuingiza katika muungano na Baba. Ni maji inayogeuka ndani mwetu Chemchem inayobubujika kwa uzima wa milele.

Ndio ee Bwana, maji inayotoka katika Moyo wako ulioyatobolewa inanifanya kuwa kiumbe kipya, mwana wa Baba na ndugu yako… *Ni maji ya ubatizo iliyomwagika juu yangu na juu ya wengi na kutufanya waana wa Mungu.*

## NJIA ZA KUPATA HURUMA YA MUNGU

Bwana YESU alimtokea Faustina alitaka wenye zambi waikimbilie Huruma ya Mungu wakati wakiwa bado hai, maana wakiisha kufa watakutana na Hukumu. Bwana Yesu kwa nyakati mbalimbali alimfundisha njia muhimu zifuatazo za kupata Huruma ya Mungu.

### 1. IBADA KWA HURUMA YA MUNGU : KUMUAMINIA NA KUMTUMAINIA KABISA YESU KRISTU

Jambo lililo kiini cha Huruma ya Mungu ni KUMWAMINIA NA KUMTUMAINIA KABISA YESU KRISTU.

Katika dunia ya leo watu hujiaminia wenyewe, Mungu hana na nafasi tena ya kwanza kama vile Muumba na Baba wa vyote. Watu uaminia shetani, akili yao, mali, cheo na kumsahau Muumbaji wa vyote hata kujitia nafasi ya Mungu. Mungu anastahili kuaminiwa sababu yeye ametuumba kwa mapendo tu. Yote tunayo ni kwa sababu ya huruma na mapendo yake. Kwa nini tunashindwa kujiachilia mikononi mwake ?

Bwana mwenyewe amemkumbusha sana jambo hili alipomwambia mtumishi wake Faustina Mtakatifu : « Hakuna roho inayoweza kutakaswa na kumpendeza Mungu isiponielekea na kuomba HURUMA YANGU ikiwa na matumaini. Wenye zambi wanielekee na kuweka tumaini lao lote kwa HURUMA YANGU. Neema huweza kuchotwa katika kilindi cha Huruma yangu kwa chombo kimoja tu, nacho ni KUNIAMINIA. Kadiri roho inavyoniaminia, kadiri hiyo hiyo itapokea. Mimi nategemea kiasi cha tumaini lako kwangu, likiwa ni kubwa, ukarimu wangu hautakua na kipimo. Zambi za KUTONIAMINIA mimi zinaniumiza sana » (PJ 50).

### 2. KUFANYA MATENDO YA HURUMA

Jambo lingine lililo ufunguo wa pili wa kupata huruma ya Mungu ni : kuwa na HURUMA KWA AJILI YA WENGINE KATIKA MATENDO, MANENO AO SALA na kazalika. Bwana Yesu alimwambia Faustina : « mtu asipotenda matendo fulani fulani ya huruma, mtu huyo hataweza kuona Huruma yangu ya mwisho. Oh ! Tafazali watu wangejua ginsi ya kukusanya azina ya Umilele (kumwaminia kabisa Kristu, kutendea wengine matendo ya Huruma). Maana kwa njia hii wataepuka kuhukumiwa wao wenyewe ; ukumu yangu itakuwa imezuiwa na matendo yao ya huruma ».

## 3. KUFANYA SIKU KUU YA HURUMA YA MUNGU

Mwaka wa 1934 Bwana Yesu alimuambia Faustina : « ninataka siku ya Mungu ya kwanza baada ya Pasaka iwe SIKU KUU YA HURUMA YA MUNGU. Siku hiyo, kilindi cha Huruma yangu kitakua wazi kwa wote. Mkristu atakayeungama na kupokea komonyo siku hiyo atapokea msamaha kamili wa zambi zake zote na wa azabu alizostahili. Wanadamu hawafurahia amani mpaka watakaponielekea wakiniaminia na kuomba Huruma yangu. Siku kuu hiyo inatokana na Huruma yangu kuu na kusabitishawa hasa katika kilindi cha Rehema na Msamaha wangu. Sikukuu hiyo ya Huruma iwe kimbilio na makao salama kwa roho za watu wote, hasa wenyi zambi. Nitamimina bahari nzima ya neema kwa wale watakaojongea chemchem ya Huruma yangu. Mtu yeyote asiogope kunikaribia, hata kama zambi zake ni nyekundu kama damu. Siku ile ya Huruma yangu, mifereji yote inayopitisha neema hufunguliwa, kwa sababu ni siku ya rehema kamili, ambao zambi zote uondolewa.

## NAMNA INAYOFAA KUSHEREA SIKUKUU YA HURUMA YA MUNGU

Bwana Yesu alimwambia Faustina Mtakatifu :

a) Siku ile ya Mungu ya pili ya Pasaka upokee komonio kwa moyo safi kabisa.
b) Kuungama (kupokea sakramenta ya Utubio - ya upatanisho), kunaweza kutangulia siku chache kabla ya siku ya Huruma.
c) Bwana Yesu akaongeza : « Siku ile ya siku kuu ya Huruma yangu, nenda mbio duniani kote (kiroho) na uzilete roho za watu wote wanaozimia kwa kuelemewa na mizigo mizito ya zambi zao, uzifikishe kwa sala kwenye chemchem ya HURUMA yangu. Nitawaponya wote na kuwatia nguvu mpya ».
d) Ninataka iwepo ibada ya « Sala Takatifu ya kuabudu Sakramenta Takatifu Eklezyani siku hiyo kwa namna ya pekee kwa nia ya kuomba Huruma kwa ajili ya dunia nzima » (kwa mwisho wa ibada ya misa).
e) Sala ya siku kenda ya kuomba Huruma ya Mungu. Bwana Yesu aliagiza kwamba SIKU KUU YA HURUMA YA MUNGU itanguliwe na sala ya siku kenda (novena) kuanzia siku ya tano takatifu. Bwana Yesu Kristu alimwambia Faustina Mtakatifu : « katika siku hizi kenda ninataka uziletee roho za watu wote kwenye chemchem ya Huruma yangu, ili zichote humo, nguvu na kitulizo, pia neema yoyote wanayoitaji katika magumu ya maisha yao, na hasa saa ile ya kufa kwao. « Katika siku hizi kenda, utaleta moyoni mwangu kundi fulani la watu, ili uwatumbukize katika Bahari ya Huruma yangu, nami nitawapeleka watu hao wote nyumbini kwa Baba yangu. Utafanya hivi katika maisha haya na katika maisha yajayo. Sitamnyima chochote mtu yule utakamletea kwenye chemchem ya Huruma yangu. Kila siku utamwomba Baba neema kwa ajili ya watu hao, na kwa mastahili ya mateso yangu makali ».

**Nia za pekee za siku hizi kenda :**

**1.** Kuombea uongofu wa dunia nzima

**4.** Kutafuta Huruma ya Mungu ijulikane popote na watu wote waweze kuutukuza wema na upendo wa Kristu Mkombozi wetu.

## 5. NAMNA YA KUFANYA IBADA ZA SIKU KENDA KWA REHEMA YA MUNGU

**(Ama Novena)**

« Yesu aliniamuru kuandika na kusali hii sala muda wa siku kenda, zitakazotangulia sikuu ya rehema ya Mungu. Itaanza siku ya tano takatifu. Muda wa siku hizo kenda nitawajalia neema ya kila namna. Ninatamani muda wa siku hizo kenda, uongoze roho kwa chemchem ya huruma yangu, kwa kuchota nguvu, unyofu na neema zote zitakazoitaji kwa kushinda magumu ya maisha, na hasa wakati wa kufa. Kila siku utauletea Moyo wangu kikundi mbalimbali cha roho utazimwaga ndani ya bahari ya huruma yangu. Nami nitaziingiza roho hizo zote ndani ya nyumba ya Baba yangu. Utatimiza utume huu muda wa maisha yako na katika umilele. Kwa ngambo yangu, sitazikatalia hata kitu kimoja, roho utakazozileta kwa kilindi cha Huruma yangu. Kila siku, kwa njia ya mateso yangu makubwa utaziombea roho hizo neema kwa Baba yangu (PJ 1209).

« Nikajibu : namna gani kusali sala hiyo ya siku kenda, roho gani kati ya roho zote nizilete kwa Moyo wako mwenyi Huruma ?»

Akanijibu hivi : « Nitakujulisha kwa siku mbalimbali » (PJ 1210-1229).

**SIKU YA KWANZA**

Maneno ya Bwana wetu Yesu Kristu : « *Leo uniletee dunia nzima, hasa wale wote wenyi zambi na uwazamishe katika bahari kuu ya Huruma yangu. Hapo utatuliza uchungu ninaupata kwa upotevu wa roho hizo*».

**Tuombe huruma kwa dunia nzima :**

Ee Yesu mwenye Huruma sana, ambaye asili ni kuwa na huruma na kutusamehe, usiangalie zambi zetu, ila imani tunayo katika uwema wako usio na mwisho. Utupokee sisi wote katika makao ya Moyo wako mwenyi Huruma na usimutupilie hata mtu mmoja mbali nawe. Tunakuomba kwa ajili ya mapendo yanayokuunga na Baba na Roho Mtakatifu.

**Wimbo :**

Ee uwezo mkubwa wa Huruma ya Mungu

Ee msaada kwa mkosefu

Uko Rehema na bahari ya Huruma

Unasaidia yeyote anayekuomba kwa unyenyekevu.

**Sala :** Baba yetu…, Nakuamkia Maria…, Sifa kwa Baba …

**Tuombe**

Ee Baba wa milele, uiangalie kwa macho ya huruma dunia nzima na kwa namna ya pekee wale wenyi zambi, wanaouaminia tu Moyo mwenye Huruma sana wa Mwanako, Bwana wetu Yesu

Kristu. Kwa ajili ya mateso yake makubwa, utuhurumie kusudi tuweze kutukuza milele hezi yako. Amen

**Kusali :**

- Shapule ya Rehema ya Mungu
- Wimbo wa sifa kwa heshima ya Huruma ya Mungu.

**SIKU YA PILI**

Maneno ya Bwana wetu Yesu Kristu : « *Leo uniletee roho za mapadri na watawa uzizamishe katika huruma yangu isiyoweza fumbulukana. Zimepata nguvu ya kuvumilia mateso yangu makubwa, na kwa njia yao, kama vile katika mifereji, huruma yangu utiririka juu ya ulimwengu* ».

**Tusali kwa ajli ya mapadri na watawa**

Ee Yesu mwenye Huruma na ambaye kwako hutoka neema zote, uzidishe neema yako ndani ya roho ya mapadri na watawa wako, ili waweze kutimiza katika ubora na heshima, tena kwa faida ya wote, matendo ya Huruma kwa ginsi wale wanaowatazama na kuzishuhudia kazi zao bora waweze kumtukuza Baba wa Huruma aliye mbinguni kwa sifa aliyostahili.

**Wimbo :**

Chemchem ya Mapendo ya Mungu inayopatikana ndani ya mioyo safi,

Ndani ya bahari ya Huruma kuna ungaro kama nyota, kama alfajiri.

**Sala :** Baba yetu…, Nakuamkia Maria, …, Sifa kwa Baba …

**Tuombe :**

Ee Baba wa milele, utupe macho ya Huruma juu ya jeshi teule ya wafanya kazi wa mzabibu wako mapadri na watawa ukiwajaza na uwingi wa baraka zako, kwa ajili ya upendo wa Moyo wa Mwana wako ambamo wameingizwa, uwape mwanga na nguvu waweze kuongoza watu katika njia ya wokovu na kusifu bila mwisho, pamoja nao, Huruma yako isiyo na mipaka na isiyoweza kufumbulikana. Amen

**Kusali :**

- Shapule ya Rehema ya Mungu
- Wimbo wa sifa kwa heshima ya Huruma ya Mungu.

**SIKU YA TATU**

**Maneno ya Bwana wetu Yesu :** *« Leo muniletee roho zote zenyi ibada na uaminifu, uzizamishe katika bahari ya Huruma yangu. Roho izo zilinituliza katika njia ya Kalvario : zilikua kama tone la kitulizo katika bahari kuu ya uchungu na mateso ».*

**Tusali kwa ajili ya wakristu wote waaminifu**

Ee Yesu mwenyi Huruma sana, unayepana kwa uwingi neema na hazina ya Huruma yako kwa watu wote, utupokee sisi wote katika makao ya Moyo wako wa Huruma tele, na usituache tutoroke humo hata mara moja. Tunakuomba tukitegemea mapendo ya ajabu na yasiyosikilika yanayowaka Moyoni kwa ajili ya Baba yako wa mbinguni.

**Wimbo :**

Maajabu ya Huruma ya Mungu hayawezi kusikilika ama kufumbuliwa wala kwa wenye zambi wala kwa waamini. Kwa wote unatupa jicho la Huruma. Unatuvuta sisi wote tuelekee Mapendo yako.

**Sala :** Baba yetu…, Nakuamkia Maria,..., Sifa kwa Baba …

**Sala**

Ee Baba wa milele, uangalie kwa macho yako ya Huruma roho aminifu, zilizo urisi wa Mwana wako, na kwa ajili ya mateso yake makubwa, uzijalie baraka zako na uzifunike kwa ukingo wa kila wakati. Usikubali zipoteze mapendo na hazina ya imani takatifu, ila uzifanyizie zisifu milele Huruma yako isiyo na mipaka pamoja na masifu ya Malaika na ya Watakatifu. Amen

**Kusali :**

- Shapule ya Rehema ya Mungu
- Wimbo wa sifa kwa heshima ya Huruma ya Mungu.

**SIKU YA NNE**

**Maneno ya Bwana wetu Yesu :**

*« Leo uniletee wapagani na wale wasionijua bado. Katika mateso yangu makubwa sana, niliwakumbuka pia, na juhudi watakaokuwa nayo baadaye ilituliza Moyo wangu. Sasa uwazamishe katika bahari kuu ya Huruma yangu ».*

**Tusali kwa ajili ya wapagani, wale wasiosadiki, na wale wasiomjua bado Kristu**

Ee Yesu mwenyi Hruma sana, Wewe uliye Mwanga wa dunia, upokee katika makao ya Moyo wako mwenye Huruma tele, roho za wapagani na za wale wasiosadiki ao wasiokujua bado. Acha myanga ya neema yako iwaangazie, kusudi, wakiungana nasi waimbe milele maajabu ya Huruma yako. Na usiwaache kutoroka mbali ya makao hayo yaliyo Moyo wako uliojaa Huruma. Amen

**Wimbo :**

Mwanga wa Mapendo yako, uangazie giza ya roho, fanya kwa ginsi roho zile zijue na zisifu pamoja nasi Huruma yako.

Baba yetu…, Nakuamkia …, Sifa kwa Baba …

**Sala**

Ee Baba wa milele, uangalie kwa huruma roho za wapagani na za wale wote wasiokujua bado. Nazo pia zimefungwa katika Moyo wa Huruma tele wa Mwana wako Bwana wetu Yesu Kristu. Uzivute kwenye mwangaza wa Enjili. Roho hizi hazijajua namna gani ni heri kubwa kukupenda. Uzifanyizie zisifu pia milele ukarimu wa Huruma yako. Amen

**Kusali :**

- Shapule ya Rehema ya Mungu
- Wimbo wa sifa kwa heshima ya Huruma ya Mungu.

**SIKU YA TANO**

**Maneno ya Bwana wetu Yesu Kristu**

« *Leo unileteе roho za waliobadirisha imani yetu na waliokana imani yetu : « Uzizamishe katika bahari kuu ya Huruma yangu. Ndizo katika mateso yangu makubwa, zilizonipasuapasua Mwili na Roho, ndio kusema Ekleya yangu. Ila wakati zitakaporudilia tena katika umoja wa Eklezya, zitaponya vidonda vyangu, nami nitasikia kitulizo katika Mateso yangu* ».

**Tusali kwa ajili ya wale waliotangatanga katika imani**

Ee Yesu mwenyi Huruma sana, uliye mwenyewe Huruma kamili na usiye wakatalia mwangaza wale wanaokuomba, pokea katika makao ya Moyo wako wa Huruma sana roho za wale waliobadilisha imani yetu, na wale waliokana imani yetu.

Kwa nguvu ya mwanga wako uzivute katika umoja wa Eklezya. Usizitupilie mbali na ukingo wako, ila ufanye kwa jinsi zisifu pia ukarimu na uwema wa Huruma yako.

**Wimbo :**

> Hata kwa wale waliopasua koti ya umoja Wako, utiririshe moyoni mwako chemchem ya Huruma, Ezi kuu ya Huruma yako, ee Mungu, inaweza kutosha roho zile ndani ya udanganyifu.

**Baba yetu…, Nakuamkia…, Sifa kwa baba.**

**Sala**

Ee Baba wa milele, angalie na macho ya Huruma roho za wale waliobadilisha imani yetu, na wale waliokana imani yetu, wale ambao wakidumu na ushupavu katika upotevu wao, wametupilia bure vipaji vyako na kupoteza bure neema zako. Usiangalie ukosefu wa shukrani na ujinga wao, ila Mapendo na Mateso makali ya Mwana wako aliyeteswa kwa ajili yao. Watu hawa pia wameingizwa ndani ya Moyo wa Yesu Mwana wako. Uwafanyizie nao pia waisifu na kuitukuza Huruma yako kubwa milele na milele. Amen.

**Kusali :**

- Shapule ya Rehema ya Mungu
- Wimbo wa sifa kwa heshima ya Huruma ya Mungu.

**SIKU YA SITA**

**Maneno ya Bwana wetu Yesu :**

« *Leo uniletee roho zilizo pole na nyenyekevu na zile za watoto wadogo ; uzizamishe katika bahari ya Huruma yangu. Roho zile, zinafanana zaidi na Moyo wangu, na ndizo zilinipatia moyo katika uchungu na mateso yangu makubwa kabla ya kufa kwangu. Niliziona kama vile Malaika wa duniani wenye kukesha na kulinda altare zangu. Juu yao namwaga neema zangu kama mito katika vilima. Neema yangu haiwezi kupokelewa ila tu na roho iliyo nyenyekevu ; roho zilizo nyenyekevu ndizo zile ninazoaminia* ».

**Tusali kwa ajili ya roho nyenyekevu na zile za watoto wadogo**

Ee Yesu mwenyi Huruma sana, uliyesema mwenyewe : « Jifunzeni kwangu kwani mimi ni mpole na mwenyi Moyo mnyenyekevu (Mt 11, 29), upokee katika makao ya Moyo wako wa Huruma tele roho pole na nyenyekevu na zile za watoto wadogo. Roho hizo zinafurahisha mbingu nzima na kupendelewa kwa namna ya pekee na Baba wa mbingu. Zipo kama fungo la maua ya harufu nzuri mbele ya kiti cha ezi cha Mungu, ambapo Mungu anafurahishwa na manukato ya fazila zao. Fanyiza zibaki daima katika Moyo wako zikiimba daima wimbo wa Mapendo na wa Huruma ya Mungu.

**Wimbo :**

> Roho zenyi kujaa unyenyekevu na upole kwa ukweli, hata ingali duniani inapumua hema ya mbinguni. Na harufu nzuri ya Moyo wake mnyenyekevu inafurahisha Muumbaji mwenyewe.

Baba yetu…, Nakuamkia…, Sifa kwa baba.

**Sala :**

Ee Baba wa milele, uangalie kwa macho ya huruma roho pole na nyenyekevu na zile za watoto wadogo zilizoingizwa katika Moyo wa Yesu unaojaa Huruma nyingi sana. Ndizo Roho zenyi kufanana zaidi na Mwana wako, kwa jinsi manukato ya roho hizo upanda kutoka hapa duniani mpaka kwenye kiti chako kitukufu.

Ee Baba wa Huruma na Mwema sana, ninakuomba basi nikitegemea Mapendo ya pekee unayo kwa ajili ya roho hizo. Baba wa huruma tele na wa uwema wote, kwa ajili ya upendo unao kwa roho hizo unazopendelea sana na zaidi, ubariki dunia nzima ili roho zote ziungane pamoja kwa kusifu Huruma yako milele na milele. Amen.

**Kusali :**

- Shapule ya Rehema ya Mungu
- Wimbo wa sifa kwa heshima ya Huruma ya Mungu.

**SIKU YA SABA**

**Maneno ya Bwana wetu Yesu**

« *Leo uniletee roho zenyi kuheshimu kwa namna ye pekee Huruma yangu, na uzizamishe katika Huruma yangu. Roho hizo ndizo zilizoshirikia zaidi mateso yangu ; pia zilipenya kabisa moyo na ufahamu wangu. Ndizo mwigo kamili na sura hai ya Moyo wangu wa huruma. Katika uzima utakaukuja, roho hizo zitameremeta kwa nuru ya pekee na hakuna moja kati yao atakayetupwa katika Jehanama na kila mmoja nitamkinga kwa namna ya pekee saa ya kufa kwake* ».

**Tusali kwa ajili ya wenye kutukuza Huruma ya Mungu**

Ee Mungu mwenyi huruma sana, wewe ambaye Moyo wako ni Mapendo, upokee katika makao ya Moyo wako wa Huruma tele roho zinazoheshimu na kutukuza kwa namna ya pekee ukubwa wa Huruma yako. Wakati wa mateso na mahangaiko yao yote, roho hizo ushinda kwa nguvu yake Mungu mwenyewe, zinatembea imara zikiaminia Huruma yako ; zinaungana na Yesu zinachukua mabegani kwao ulimwengu wote. Roho hizo hazitahukumiwa kwa ukali, lakini Huruma yako itawazunguka wakati wa kufa kwao.

**Wimbo :**

Roho inayosherehe uwema wa Bwana wake, inapendelewa naye. Roho ile ni kila mara karibu ya chemchem ya uzima, na inachota neema ndani ya Huruma ya Mungu.

**Baba yetu…, Nakuamkia…, Sifa kwa Baba.**

**Sala :**

Ee Baba wa milele, uangalie kwa macho ya Huruma roho zinazotukuza, kwa juhudi na upendo wa pekee, na kusifu, hasa tabia yako kubwa na ya kwanza, yaani Huruma yako isiyo na mipaka – roho hizo zinafichwa katika Moyo wa huruma mno wa Yesu. Roho hizo ni kama Enjili hai. Mikono yao inajaa matendo ya huruma, na mioyo yao, ikijazwa na furaha inaimba wimbo wa sifa ya Huruma yako.

Tunakuomba, ee Mungu Mwema, uwaonee huruma kadiri ya matumaini wanayo na kukuaminia wewe tu, ili kwa njia hiyo, litimie Agano la Mwokozi akisema : « *roho zitakazotukuza huruma yangu isiyo na mipaka, nitazilinda mimi mwenyewe kama sifa yangu ya pekee muda wa maisha yao na hasa saa ya kufa kwao* ». Amen

**Kusali :**

- Shapule ya Rehema ya Mungu
- Wimbo wa sifa kwa heshima ya Huruma ya Mungu.

## SIKU YA NANE

**Maneno ya Bwana wetu Yesu**

*« Leo uniletee roho zinazofungwa katika gereza ya matoharani na uzizamishe ndani ya kilindi cha huruma yangu, ili vijito vya damu yangu, vitulize vidonda vyao vya kuunguzwa kwa moto. Roho hizo zote upendwa nami sana mno. Zipo matoarani kwa ajili ya kulipa Haki yangu sababu ya kunikosea hapa duniani. Wewe lakini una uwezo wa kuwapatia kitulizo fulani. Inakupasa wewe kuchota Rehema zote katika hazina ya Eklezya yangu na kuzitolea kwa ajili yao ».*

*Oh ! Ungalijua tu masumbuko yao na ukali wa mateso yao, haungeliacha kutolea kila mara sadaka ya roho yako, na ungezilipia deni zao kwa haki yangu.*

**Tusali kwa ajili ya roho za matoharani**

Yesu mwenye Huruma sana ulisema ya kuwa unataka huruma, tazama, naleta katika makao ya Moyo wako wa huruma sana, roho za matoarani unazopendelea sana, lakini zinazopashwa kulipa deni wanazo mbele ya Haki yako : vijito vya Damu na Maji vilivyotiririka kutoka moyoni mwako vizimishe ndimi za moto wa matoharani ili hapo pia utukuzwe uwezo wa huruma yako. Amen.

**Wimbo :**

> Kutoka ukali wa kutisha wa moto wa matohara, mlio upanda kulalamikia Huruma yako, na ndipo watulizwa na mishale ya moto inazimishwa kwa ajili yao kupitia mito ya maji yenyi kuchanganyiwa na damu yako.

**Baba yetu…, Nakuamkia…, Sifa kwa Baba.**

**Sala**

Ee Baba wa milele, utupe macho ya Huruma juu ya roho zenyi kuteswa katika matohara. Nao pia wameingizwa katika Moyo wa Yesu, mwenye Huruma sana. Nakusihi kwa mastahili ya mateso makubwa ya Yesu Mwana wako, na kwa uchungu mkali uliojaza Roho yake Mtakatifu, uonyeshe Huruma yako roho zile unazoziangalia kwa haki ; usiziangalie namna ingine ila tu kupitia vidonda vya Yesu Mwanao mpendelevu sana kwa kuwa tunasadiki ya kwamba uwema na Huruma yako havina mipaka. Amen

**Kusali :**

- Shapule ya Rehema ya Mungu
- Wimbo wa sifa kwa heshima ya Huruma ya Mungu.

**SIKU YA KENDA**

**Maneno ya Bwana wetuYesu**

*« Leo uniletee Roho za wale waliokwisha ingiya katika hali ya uvuguvugu na uzi*zamishe *katika kilindi cha Huruma yangu. Roho hizo ndizo zaumiza sana Moyo wangu kila wakati. Katika bustani ya Mizeituni, nilichukizwa zaidi sana, tena mno, na roho moja niliyoona hainihangaikii wala kunishurulikia. Ndipo nililia juu ya roho ile moja tu, nilisema kwa uchungu tele : « Ee Baba, upitishe mbali nami kikombe hiki, ikiwa ndivyo mapenzi yako. » Kwao njia ya mwisho ya wokovu wao ni kukimbilia huruma yangu »*

**Tusali kwa ajili ya roho zilizo vuguvugu**

Ee Yesu mwenye Huruma nyingi sana. Wewe uliye tu huruma yenyewe, roho zile zilizo kama barafu, uzipokee ndani ya makao ya Moyo wako ulio na huruma bila kipimo. Roho hizo ni kama mizoga zenyi kufanana na maiti na zinazokuchukiza sana. Fanyiza, twakuomba sana, uziingize katika moto wa upendo wako safi sana, ili ziote moto.

Ee Yesu mwenye Huruma kubwa mno, tumia uwezo wa Huruma yako, na uzivute katikati ya moto yenyewe ya mapendo yako tena uzijalie mapendo ya Mungu kwa sababu unaweza vyote.

**Wimbo :**

> Moto na barafu haviwezi kuchangwa pamoja sababu ao moto utazimika ao barafu itayeyuka. Lakini huruma yako, ee Mungu wangu inaweza kuchukua uharibifu mkali hata zaidi.

**Baba yetu…, Nakuamkia…, Sifa kwa baba**

**Sala**

Ee Baba wa milele, uangalie kwa macho ya huruma roho zenyi uvuguvugu, ambazo katika hali yao hiyo, wameingizwa ndani ya Moyo wa Huruma sana wa Mwana wako Bwana wetu Yesu Kristu.

Ee Baba wa Huruma, tunakusihi kwa mastahili ya mateso makali sana ya Mwana wako, na hasa kwa mateso yake ya mwisho aliyovumilia pale msalabani muda wa saa tatu mbele ya kufa, uzifanyizie nazo pia zitukuze kilindi cha Huruma yako milele na milele. Amen.

**Kusali :**

- Shapule ya Rehema ya Mungu
- Wimbo wa sifa kwa heshima ya Huruma ya Mungu.

**Angalisho**

Inashauriwa sana kusali sala za siku kenda katika matukio yote ya lazima ya maisha. Tunashauriwa pia sana wakati wa sala za siku kenda kushirikia sakramenta ya Ukaristia na ya Utubio na kutenda Matendo ya mapendo. Sala hii ya kuomba inayompendeza Mwokozi mwema

ni ya mafaa kwa kupata neema za ajabu za kiroho na za kimwili. Tena yule anayeweza tafazali afunge chakula jinsi anavyotaka na kujikatalia katika mambo mbalimbali ya furaha za mwili, hasa kwa kiroho, kupiganisha vilema mbali mbali.

**SHAPULE YA REHEMA YA MUNGU**

**Ahadi ya Bwana wetu Yesu Kristu**

*« Nitazigawiya neema kubwa sana roho zile zitakazo sali shapule hii. Zitafunikwa na Huruma yangu muda wa maisha yao na hasa siku ya kufa ».* (PJ 574)

1. **Namna ya kusali**

Unatumia shapule ya desturi. Kiisha unasali hivi :

- Baba yetu
- Nakuamkia Maria
- Sala ya kusadiki

2. **Juu ya punje nene, unasema mara moja :**

Baba wa milele, ninakutolea Mwili na Damu, Roho na Umungu wa Mwana wako Mpenzi, Bwana wetu Yesu Kristu kwa malipo ya zambi zetu na za dunia nzima.

3. **Juu ya punje ndogo, unasema mara kumi**

Kwa ajili ya mateso yake makubwa utuhurumie sisi na uhurumie dunia nzima.

4. **Kwa kumaliza unasema mara tatu**

Mungu Mtakatifu, Mungu wa nguvu, Mungu wa milele utuhurumie sisi na uhurumie dunia nzima.

5. **Kiisha utasali sala ya kwanza :**
   Eee Damu na maji vilivyotiririka kutoka moyo wa Yesu kama chemchem ya huruma kwa ajili yetu, tunakuaminia. (Unasali mara tatu)

6. **Sala ya pili**

Ee Mungu ambaye huruma haina mwisho na ambaye hazina za huruma haziwezi kukauka, utuangalie kwa macho yako ya huruma, uzidishe ndani mwetu huruma yako kusudi tusipoteze matumaini hata katika majaribu makuu ; lakini tukiwa na matumaini makuu, tufwate siku zote mapenzi yako matakatifu ambayo ni mapendo na huruma. Kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristu, Mfalme wa huruma, ambaye pamoja nawe na Roho Mtakatifu anatujalia huruma yake milele na milele. Amen

**Wimbo wa Sifa kwa heshima ya Huruma ya Mungu**

- Huruma ya Mungu fumbo lisilosikilika la Utatu Mtakatifu *Ninakuaminia*
- Huruma ya Mungu, hakikisho la Ukubwa wake mkuu sana,
- Huruma ya Mungu uliyeumba Roho za mbingu
- Huruma ya Mungu uliyetuita kuwapo japo hatukukuwa
- Huruma ya Mungu uliyeunda ulimwengu mzima
- Huruma ya Mungu uliyetupatia uzima wa milele
- Huruma ya Mungu uliyetuepusha azabu tuliyostahili
- Huruma ya Mungu uliyetutosha katika mauti ya zambi
- Huruma ya Mungu uliyeshuka duniani katika fumbo la Neno aliyejifanya mtu
- Huruma ya Mungu uliyetoka katika vidonda vya Kristu
- Huruma ya Mungu uliyetiririka kutoka Moyo Mtakatifu wa Yesu
- Huruma ya Mungu uliyetupatia Bikira Mtakatifu sana kuwa Mama wa huruma
- Huruma ya Mungu uliyeonekana katika kusimikwa kwa Eklezia ya dunia nzima
- Huruma ya Mungu uliojionyesha katika kusimika na kutumia Sakramenta Takatifu
- Huruma ya Mungu usiye na mwisho katika Sakramenta za Ubatizo na Utubio
- Huruma ya Mungu usiye na kipimo katika Sakramenta za altare na Upadirisho
- Huruma ya Mungu unayetuita kwa Imani takatifu
- Huruma ya Mungu utakaso wa wanyofu
- Huruma ya Mungu katika ukamilifu wa wenye bidii
- Huruma ya Mungu afya ya wagonjwa na ya wenye kuteswa
- Huruma yaMungu kitulizo cha mioyo yenye shida
- Huruma ya Mungu matumaini ya waliopoteza matumaini
- Huruma ya Mungu unayetusindikiza siku zote na popote
- Huruma ya Mungu unayetangulia na neema zako
- Huruma yaMungu Amani yawenye kuzimia roho
- Huruma ya Mungu unayetuhepusha moto wa jehanama
- Huruma ya Mungu unayetuliza roho za matoarani
- Huruma ya Mungu furaha na raha ya watakatifu wote
- Huruma ya Mungu usio na mwisho katika mafumbo yote ya Imani
- Huruma ya Mungu, usiyeweza kukauka katika miujiza.

Mungu ni mwenye huruma na mpole, Mvumilivu na mwenye wema mwingi.

Ndio sababu nitaimba milele huruma ya Bwana.

**Tuombe**

Eee Mungu ambaye huruma haina mwisho na ambaye hazina za huruma haziwezi kukauka, utuangalie kwa macho yako ya huruma, uzidishe ndani mwetu huruma yako kusudi tusipoteze matumaini hata katika majaribu makuu ; lakini tukiwa na matumaini makuu, tufwate siku zote mapenzi yako matakatifu ambayo ni mapendo na huruma. Kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristu, Mfalme wa huruma, ambaye pamoja nawe na Roho Mtakatifu anatujalia huruma yake milele na milele. Amen

**SALA YA KUOMBA NEEMA YA KUWA NA HURUMA KWA WENGINE (PJ 163)**

Kwa kila pumzi ya maisha yangu, kila mpigo la moyo wangu, na kila mara damu yangu inavyosukumwa mishipani mwangu, ndivyo natami kila mara kutukuza Huruma yako, ee Utatu Mtakatifu sana.

Natamani kujigeuza mimi mzima kuwa Huruma yako, na niwe hivi ungaro kamili ya Wewe mwenyewe, ee Bwana. Fanya kwa jinsi hali kubwa zaidi ya Mungu, yaani huruma yake isiyo na mipaka, imiminike kutoka roho na moyo wangu kumfikia jirani yangu.

Unisaidie, ee Bwana, ili macho yangu yajazwe huruma, ili hata mara moja nisimhukumu ao kumwazia mtu kufuatana tu jinsi anavyoonekana nje, bali nivumbue ubora ulio katika roho ya mwenzangu ao jirani na niweze kumsaidia.

Unisaidie, ee Bwana, ili masikio yangu, yajazwe huruma, ili nishurulikie mahitaji ya jirani yangu na nisibaki bila kuhangaikia magumu yake, wala malalamiko yake, bali nimsaidie kadiri niwezavyo.

Unisaidie, ee Bwana, ili kinywa changu kijazwe huruma, kwa jinsi, hata mara moja nisimsingizie jirani yangu, ila nimwambie kila mmoja maneno ya kumtuliza na ya kumsamehe.

Unisaidie, ee Bwana, ili mikono yangu iwe yenye huruma, na ijaliwe matendo mema, ili nisiache kamwe, kumtedea jirani mema, na nijitwike kazi nzito na zenyi kuchukiza.

Unisaidie, ee Bwana, ili miguu yangu iwe yenyi huruma, kwa ginsi nijiharikishe kila mara kumsaidiya jirani yangu, nikishinda uregevu wangu na mchoko wangu. Pumziko langu la kweli liwe kumtumikia jirani yangu.

Unisaidie, ee Bwana, ili moyo wangu ujazwe huruma sana, ili niguswe na mateso yote ya jirani yangu. Nisimkatalie hata mtu mmoja kumpa moyo wangu. Nitawaendea bila unafiki hate wale ambao najua kwamba watautumia vibaya uwema wangu, nami nitajifungia peke yangu katika Moyo wa Huruma sana wa Yesu. Nitanyamaza juu ya mateso yangu mwenye. Huruma yako ikae ndani mwangu, ee Bwana wangu.

Wewe ndiwe unayeniamuru nijizoeshe katika daraja tatu za Huruma: ya kwanza - Kitendo cha Huruma haizuru aina gani; ya pili - Neno la Huruma: nisipoweza kusaidiya katika matendo, nitasaidia kwa njia ya maneno; ya tatu - Nisipoweza kushuhudia Huruma wala kwa matendo, wala kwa maneno nitaweza kuifanya kwa sala. Natuma sala zangu hata popote ninapozuiwa kufikia kimwili. (PJ 163).

## SALA YA KUJITOLEA KWA YESU MWENYE HURUMA

Ee Yesu mwenyi huruma sana, huruma yako aina mwisho na hazina za neema zako haziwezi kuisha. Ninayo matumaini yasiyo na mipaka kwa huruma yako inayopita matendo yote.

Najitolea kwako kabisa bila kujiwekea chochote, ili niishi na nitafute ukamilifu wa kikristu chini ya myanga iliyotiririka kutoka Moyo wako Mtukufu uliyotobolewa msalabani.

Natamani kutangaza huruma yako, nikitimiza matendo ya huruma ya kiroho na ya kimwili, hasa kwa ajili ya kuongoka kwa wenye zambi, kusaidia maskini, kuwatuliza wenye uzuni na wagonjwa, kuwaombea wanaozimia roho na roho zenye kuteswa matoharani.

Unilinde mimi kama vile yule anayepashwa kutumikia sifa yako, sababu naogopa vyote vitokavyo katika uzaifu wangu, ila ninatumaini kupata vyote kwa huruma yako isiyoweza kumalizika. Ee Mwokozi Mwema, tafazali ulimwengu nzima ujue kilindi kisichoweza kusikilika cha huruma yako, nao uaminie uwezo wake mkuu na kuitukuza hapa duniani na milele. Amen.

**Yesu ninakutumainia (x3)**

## TOLEO KWA MUNGU

“Ee Yesu, ambaye mapendo isiyo na mipaka yaliumba na kuikomboa dunia tena kutamani kuiokoa, unipokee katika hesabu ya wale wanaotaka kutumikia ushindi na shangwe ya Ufalme wa Mapendo yako duniani.

Kwa ajili ya ukomo huo, upokee matoleo yangu mimi mzima ninayejitolea kwa kazi yako.

Ee Yesu, tenda miujiza ya watu wenye kuongoka moyoni! Uwaite mitume kwa nyakati za sasa, mitume wapya kwa kazi hiyo kubwa sana.

Uijaze dunia nzima na uwingi wa Mapendo ya Huruma yako kwa jinsi, ubaya ukizikwa, ukibomolewa na kuvujwa, dunia itageuka kuwa tena mpya; na mioyo inayojazwa mapendo ilete na kuvuta wafuasi wa Enjili wakiwa kama vile mwanga wa pambazuko. Yesu mwenye huruma, **tunakusadikia na tunakuaminia**. Njoo utusaidie katika umaskini na uzaifu wetu. Utufanyizie tuweze kukujulisha na kukupendesha kwa watu wote.

Tukisadikia na kuaminia uwingi wa mapendo yako, tunataka kupiganisha mabaya ndani mwetu na duniani kote kwa ajili ya sifa yako na wokovu wetu. Amen

## AGIZO

Ee Yesu wangu, unichunge pembeni yako, na usiruhusu nijitenge nawe, angalia uzaifu wangu, bila wewe siwezi kufanya hata hatua moja. Ee Yesu, inafaa basi uwe pamoja nami kama vile mama asiyeacha mtoto wake mchanga, na hata zaidi ya ile, yeye akimwacha, ninayo matumaini kamili, wewe hautaniacha kamwe.

**KUABUDU UKARISTIA TAKATIFU**

1. Wimbo wa ukaristia
2. Kulinda ukimya – kujiweka mbele ya Mungu
3. Neno la Mungu – fikara
4. UKIMYA – kuabudu Yesu Kristu mzima katika ukimya
5. Maombi
6. Tantum ergo

    Sakramenta kubwa hiyo
    Tuabudu kifudii
    Na sheria ya zamani
    Ikomeshwe na hiyo
    Tusipoona kwa macho
    Tuisadiki kwa imani
    Sifa shangwe sala na heshima
    Na ezi nayo baraka
    Kwake Baba kwake Mwana
    Naye Roho Mtakatifu
    Atokaye kwa wawili
    Iwe pia sifa sawa. Amen

7. Baraka kuu (kama kuko Padri)
8. Masifu :

    Mungu atukuzwe
    *Litukuzwe jina lake Takatifu*
    Atukuzwe Yesu Kristu
    *Mungu kweli na mtu kweli*
    Litukuzwe jina la Yesu
    *Utukuzwe Moyo wake Mtakatifu sana*
    Atukuzwe Yesu Kristu
    *Itukuzwe damu yake Takatifu sana*
    Atukuzwe Yesu Kristu
    *Katika Sakramenta kuu ya altare*
    Atukuzwe Roho Mtakatifu
    *Baba mwenyi kuleta uzima*
    Atukuzwe Roho mufariji
    *Mwenyi kutoka kwa Baba na Mwana*
    Atukuzwe Mama Mtukufu wa Mungu
    *Bikira Maria Mtakatifu*
    Atukuzwe Bikira Maria
    *Aliyekingiwa na zambi ya asili*
    Atukuzwe Bikira Maria
    *Aliyepalizwa Mbinguni*
    Litukuzwe jina la Maria
    *Bikira na Mama*

Atukuzwe Yusufu Mtakatifu

*Mume wake wa usafi bora*

Atukuzwe Mungu

*Katika Malaika na watakatifu wake wote.*

*Ndivyo !*

*Ndivyo !*

9. Kurudisha ukaristia Takatifu ndani ya tabernakulo (katika ukimya).
10. Wimbo wa mwisho kiisha kurudisha Ukaristia ndani ya tabernakulo (wimbo wa Mama Maria).

**SALA KWA AJILI YA ROHO ZA MATOARANI**

**Mwendo wa sala**

Ingilo : Wimbo wa mwanzo.

- Alama ya Msalaba
- Nia ya sala
- Sala ya mwanzo
- Shapule ya kawaida ao Shapule ya Rehema ya Mungu
- Neno la Mungu
- Maombi
- Litania kwa ajili ya roho za matoarani
- Sala : Salamu Malkia
- Zaburi 129 (De profondis)
- Sala kwa ajili ya roho za matoarani
- Wimbo

**Sala ya mwanzo : Tusali kwa ajili ya roho za matoharani**

Yesu mwenye Huruma sana ulisema ya kuwa unataka huruma, tazama, naleta katika makao ya Moyo wako wa huruma sana, roho za matoarani unazopendelea sana, lakini zinazopashwa kulipa deni wanazo mbele ya Haki yako : vijito vya Damu na Maji vilivyotiririka kutoka moyoni mwako vizimishe ndimi za moto wa matoharani ili hapo pia utukuzwe uwezo wa huruma yako. Amen.

**Litania kwa ajili ya roho za matoarani**

- Bwana utuhurumie,
- Kristu utuhurumie
- Bwana utuhurumie
- Kristu utusikie
- Kristu utusikilize,
- Baba wa mbingu Mungu, *uwahurumie roho za matoarani*
- Mwana Mkombozi wa dunia Mungu, *uwaruhumie roho za matoarani*
- Roho Mtakatifu Mungu, *uwahurumie roho za matoarani*

- Utatu Mtakatifu Mungu mmoja, *uwahurumie roho za matoarani*
- Maria Mtakatifu, Mama wa Mungu, *uwaombee roho za matoarani*
- Mtakatifu Mikaeli Malaika Mkuu, *uwaombee roho za matoarani*
- Malaika mlinzi wangu na malaika wa roho za matoarani, *muwaombee*
- Jeshi la wamalaika wa mbingu, *muwaombee*
- Yusufu Mtakatifu na Yoane Mbatizaji mtakatifu, *muwaombee*
- Enyi Mababu wetu wa imani na Manabii, *muwaombee*
- Petro na Paolo watakatifu, *muwaombee*
- Enyi Mitume na Waenjili watakatifu, *muwaombee*
- Stefano na Lorenzio watakatifu, *muwaombee*
- Enyi watakatifu Mashahidi, *muwaombee*
- Gregorio na Agostino watakatifu, *muwaombee*
- Enyi Walimu wa Eklezya, wa Papa na Waungamadini watakatifu, *muwaombee*
- Anna na Maria Madalena watakatifu, *muwaombee*
- Enyi Mabikira na Wajane watakatifu, *muwaombee*
- Enyi watakatifu wote wa Mbingu, *muwaombee*
- Utufanyizie kwa wema, *Uwahurumie Bwana*
- Utufanyizie kwa wema, *Utusikilize ee Bwana*
- Kwa ajili ya jina Tukufu la Yesu, *Uwahurumie roho za matoarani*
- Kwa ajili ya Rehema yako kubwa, *Uwahurumie roho za matoarani*
- Kwa ajili ya Mateso yako makali na kwa ajili ya Kufa kwako, *Uwahurumie roho za matoarani*
- Kwa ajili ya Damu yako na kwa vidonda vyako vitukufu, *Uwahurumie roho za matoarani*
- Sisi wakosefu, *twakuomba utusikie*
- Ukubali kuwahurumia marehemu wote, *twakuomba utusikie*
- Ukubali kutuliza ugumu wa maamzi yako, *twakuomba utusikie*
- Ukubali kuwachukua katika mahali pa Amani na ya pumziko ya milele, *twakuomba utusikie*
- Ukubali wapokee urisi wa Baba, *twakuomba utusikie*
- Ukubali waone uzuri wa ungaro wako, *twakuomba utusikie*
- Ukubali kuwasharikisha na uwingi wa wema wako, *twakuomba utusikie*
- Ukubali kutimiza hamu yao ya wokovu, *twakuomba utusikie*
- Ukubali kawajalia pumziko hasa mioyo ya wazazi wetu, marafiki na wafazili wetu wote, *twakuomba utusikie*
- Ukubali kuwajalia rehema yako roho zenyi hazina watu wa kuwaombea, *twakuomba utusikie*
- Ufanye ili sadaka ya Misa na Komonyo takatifu inayotolewa kwa ajili yao iwe msaada kwao, *twakuomba utusikie*
- Mwana Kondoo wa Mungu unayeondowa zambi za dunia, *uwahurumie ee Yesu mwema*
- Mwana Kondoo wa Mungu unayeondowa zambi za dunia, *uwasikilize ee Yesu mwema*
- Mwana Kondoo wa Mungu, unayeondowa zambi za dunia, *uwajalie marehemu hawa pumziko la milele*

**Salamu Malkia**

Salamu Malkia,
Mama mwenye huruma
Wee uzima wetu
Kitulizo na kitumaini chetu, salamu.
Tunakulilia, sisi waana maskini wa Eva,
Tunakutumainia, tukilalamika na kulia humu katika inchi ya machozi.
Haya, basi, Mwombezi wetu,
Ututazamie kwa macho yako ya huruma
Tutakapo toka ugenini hapa,
Utuonyeshe mzao Mbarikiwa wa tumbo lako Yesu.
Ee Bikira Maria mwenye Huruma, ee Bikira Mwema, ee Bikira Mpole.

**Zaburi 129**

Toka chini nakulia, ee Bwana
Ee Bwana, usikie sauti yangu

Masikio yako yasikilize
Sauti ya maombi yangu.

Ukikumbuka zambi zangu, ee Bwana
Ee Bwana, nani atasimama ?

Lakini kwako kuna maondoleo
Ili wakutumikie kwa furaha.

Ninamtumainia Bwana,
Roho yangu inatumaini,
Ninangojea Neno lake.

Roho yangu inangojea Bwana
Kuliko walinda zamu
Wanavyongojea asubui.

Eee Israeli, umngojee Bwana
Kwa maana kwa Bwana kuna huruma
Kwake kuna wokovu mwingi.

Yeye atatoa Israeli

Katika maovu yake.

- **Sala ya mwisho**

Ee Bwana Yesu, uwahurumie roho zinazoteswa matoarani.
Kwa ajili ya kuwakomboa ulichukua mwili wa binadamu
Ukikubali kuteswa vikali sana ata kufa Msalabani.
Angalia kwa macho ya huruma tamaa yao ya kukuona.
Angalia machozi yao ya kitubio.
Kwa ajili ya mateso yako makubwa,
Uwahurumie mateso wanayostahili sababu ya zambi zao.
Ee Yesu mpole sana,
Ufanye damu yako ishuke na imwagike juu ya mioyo hiyo,
Ifupishe muda wao wa utakaso
Ili wachukuliwe kwako bila kukawia
Wapate kurisi karibu nawe uzima wa milele. Amen !

- Wimbo

## 1. FIKARA YA NENO LA MUNGU

1. Wimbo
2. Sala
3. Kualika Roho Mtakatifu
4. Kusoma Neno la Mungu
   Kusoma mara mbili hao mara tatu
5. Kutoa misemwa ao kipindi iliyotugusa kiisha kusikia Neno la Mungu
6. Ukimya
   Kuacha Mungu aseme katika ukimya wa roho.
7. KUGAWANYA
   Kugawa yale maneno haya yanaamsha ao kumaanisha katika maisha yangu ya imani.
8. Kutoa sala
9. Makusudio ya kundi : tendo la kundi kufuatana na Neno la Mungu tuliofikiri na kusali
10. Sala ao wimbo
    Kumaliza na wimbo ao sala inayojulikana na kundi.

## ROZARYO TAKATIFU

### Mwendo wa sala

- Alama ya msalaba
- Sala ya kusadiki
- Sala ya Baba yetu
- Sala ya Nakuamkia Maria(x3)
- Sifa kwa Baba na kwa Mwana

***Yanatajwa matendo ya siku katika juma, kiisha kutaja kila tendo, twasali Baba yetu mara moja na Nakuamkia Maria mara 10 mwisho***.

Sifa kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, kama ilivyo kuwa mwanzo na sasa na siku zote na miaka ya milele. **Amen**.

***Tunaongeza*** : Uje Roho Mtakatifu, uje kwa nguvu na maombezi ya Bikira Maria, mchumba wako wa usafi bora.

Ee Yesu mwenye huruma ***:*** utusamehe makosa yetu, utuepushe na moto wa jehanama na upeleke roho zote mbinguni, hasa zile zinazokuwa na lazima sana ya huruma yako. Amen.

### MATENDO YA FURAHA

(Siku ya kwanza na ya sita)

❖ **Tendo le kwanza la furaha** :

Tumkumbuke Maria alipoelezwa kama atakuwa Mama wa Mwokozi, na tuombe neema ya unyenyekevu.

- Tendo la pili la furaha :

Tumkumbuke Maria alipo mwendeya Elizabeti Mtakatifu na tuombe neema ya kupenda vema watu.

- **Tendo la tatu la furaha** :

Tumkumbuke Maria alipo mzaa mtoto Yesu, na tuombe neema ya kuvumilia vema umaskini wetu.

- **Tendo la nne la furaha** :

Tumkumbuke Maria alipomtolea mtoto Yesu hekaluni, na tuombe neema ya usafi wa moyo.

- **Tendo la tano la furaha** :

Tumkumbuke Maria alipomkuta Yesu Hekaluni, na tuombe neema ya utii.

## MATENDO YA MWANGAZA

(Siku ya nne)

- **Tendo la kwanza la mwangaza** :

Tumkumbuke Yesu alipobatizwa katika Yordani ; na tuombe neema ya kuheshimu maagano ye Ukristu.

- **Tendo la pili la mwangaza** :

Tumkumbuke Yesu alipogeuza maji kuwa divai pa Kana, na tuombe neema ya kumkimbilia Kristu kila wakati.

- **Tendo la tatu la mwangaza** :

Tumkumbuke Yesu alipowaalika watu waongoke moyoni na kuamini Habari Njema, na tuombe neema ya wokovu kamilifu.

- **Tendo la nne la mwangaza** :

Tumkumbuke Yesu alipogeuka sura ; na tuombe neema ya kugeuka watu wapya katika Kristu.

- **Tendo la tano la mwangaza** :

Tumkumbuke Yesu alipofanya Ukaristia Takatifu chakula cha uzima wa milele na alama ya mapendo yake ; na tuombe neema ya kupokea katika hali nzuri mwili wa Kristu.

## MATENDO YA UCHUNGU

(***Siku ya Pili na ya Tano***)

- **Tendo la kwanza la uchungu** :

Tumkumbuke Yesu alipotoka jasho la damu katika bustani ya mizeituni ; na tuomne neema ya kusikitika vema kwa zambi zetu.

- **Tendo la pili la uchungu** :

Tumkumbuke Yesu alipopigwa mijeledi na waaskari, na tuombe neema ya kukimbiya furaha za mwili.

- **Tendo la tatu la uchungu** :

Tumkumbuke Yesu alipotiliwa taji la miiba kichwani ; na tuombe neema ya kuacha kiburi.

- **Tendo la nne la uchungu** :

Tumkumbuke Yesu alipochukuwa msalaba wake ; na tuombe neema ya kuvumilia mateso yetu.

- **Tendo la tano la uchungu** :

Tumkumbuke Yesu aliposulubiwa ; na tuombe neema ya kupenda Yesu na Maria.

## MATENDO YA UTUKUFU

(***Siku ya tatu na ya Mungu***)

- **Tendo la kwanza la utukufu** :

Tumkumbuke Yesu alipofufuka ; na tuombe neema ya usabiti wa imani.

- **Tendo la pili la utukufu** :

Tumkumbuke Yesu alipopanda mbinguni ; na tuombe neema ya usabiti wa kitumaini.

- **Tendo la tatu la utukufu** :

Tumkumbuke Yesu alipowatumiya Mitume Rogho Mtakatifu ; na tuombe neema ya usabiti wa mapendo.

- **Tendo la nne la uchungu** :

Tumkumbuke Maria alipopalizwa mbinguni ; na tuombe neema ya kufa kuzuri.

- **Tendo la tano la utukufu** :

Tumkumbuke Maria alipopokelewa mbinguni ; na tuombe neema ya kukaa sikuzote katika katika wema.

**Salamu Malkia** : Mama mwenyi huruma, ewe uzima wetu kitulizo na kitumaini chetu, salamu. Tunakulilia sisi waana wa maskini wa Eva, wenyi kukaa ugenini. Tunakutumainia, tukilalamika na kulia huku, katika nchi ya machozi. Haya bashi, Mwombezi wetu, ututazamiye kwa macho yako ya huruma. Tutakapo toka ugenini hapo, utuonyeshe Mzao mbarikiwa mtoto wa tumbo lako, Yesu. Ee Bikira Maria mwenyi huruma, ee Bikira mwema, ee Bikira mpole. **Amen**.

**Litania za Bikira Maria Mtakatifu**

| | |
|---|---|
| Bwana utuhurumie, | Bwana utuhurumie |
| Kristu utuhurumie, | Kristu utuhurumie |
| Bwana utuhurumie, | Bwana utuhurumie |
| Kristu utuhurumie, | Kristu utuhurumie |
| Baba wa mbinguni Mungu, | Utuhurumie |
| Mwana Mkombozi wa dunia, Mungu, | Utuhurumie |
| Roho Mtakatifu, Mungu, | Utuhurumie |
| Utatu Mtakatifu, Mungu mmoja, | Utuhurumie |
| Maria Mtakatifu, | Utuombee |
| Mzazi Mtakatifu wa Mungu, | Utuombee |
| Mama mwenyi moyo safi, | Utuombee |
| Mama usiye na zambi, | Utuombee |
| Mama usiye na taka, | Utuombee |
| Mama mpendelevu, | Utuombee |
| Mama mzuri sana, | Utuombee |
| Mama wa shauri njema, | Utuombee |
| Mama wa Muumba, | Utuombee |
| Mama wa mwokozi, | Utuombee |
| Bikira mwenye utaratibu, | Utuombee |

| | |
|---|---|
| Bikira mwenye heshima, | Utuombee |
| Bikira mwenye sifa, | Utuombee |
| Bikira mwenye uwezo, | Utuombee |
| Bikira mwenye huruma, | Utuombee |
| Bikira mwamini, | Utuombee |
| Kioo cha haki, | Utuombee |
| Kikao cha hekima, | Utuombee |
| Sababu ya furaha yetu, | Utuombee |
| Chombo cha neema, | Utuombee |
| Chombo cha heshima, | Utuombee |
| Chombo bora chai bada, | Utuombee |
| Waridi wa fumbo, | Utuombee |
| Mnara wa Daudi, | Utuombee |
| Mnara wa pembe, | Utuombee |
| Nyumba ya zahabu, | Utuombee |
| Sanduku ya Agano, | Utuombee |
| Mlango wa Mbinguni, | Utuombee |
| Nyota ya asubui, | Utuombee |
| Afya ya wagonjwa, | Utuombee |
| Makimbilio ya wakosefu, | Utuombee |
| Mtulizaji wa wenye uchungu, | Utuombee |
| Msaada wa wakristu, | Utuombee |
| Malkia wa Malaika, | Utuombee |
| Malkia wa Mababu, | Utuombee |
| Malkia wa Manabii, | Utuombee |
| Malkia wa Mitume, | Utuombee |
| Malkia wa wafiadini, | Utuombee |

Malkia wa waungama dini, Utuombee

Malkia wa Mabikira, Utuombee

Malkia wa watakatifu wote, Utuombee

Malkia uliyekingiwa na zambi ya asili, Utuombee

Malkia uliye twaliwa mbinguni, Utuombee

Malkia wa Rozaryo takatifu, Utuombee

Malkia wa waamini, Utuombee

Malkia wa Amani, Utuombee.

Mwana kondoo wa Mungu unayeondowa zambi za dunia,
***Utuondolee Bwana***

Mwana kondoo wa Mungu unayeondowa zambi za dunia,
***Utusikilize Bwana***

Mwana kondoo wa Mungu unaye ondowa zambi za dunia. ***Utuhurumie***.

**Utuombee sisi, Mzazi mtakatifu wa Mungu** : Tupate kustahili ahadi zake Kristu.

**Tuombe** : Ee Bwana Mungu, tunakuomba : utujalie sisi watumishi wako tuwe daima na afya ya roho na ya mwili ; na kwa maombezi matukufu ya Maria Mtakatifu, Bikira siku zote, tupone katika uchungu wa sasa, na kupata furaha ya milele. Kwa ajili ya Bwana wetu. **Amen**.

- Roho za marehemu kwa neema ya Mungu, wapumzike kwa amani ;
- Na mwanga wa milele uwaangazie.

➢ **Sala kwa Mtakatifu Mikaeli Malaika Mkuu**

Mtakatifu Mikaeli, Malaika Mkuu ; utulinde katika mapigano ; uwe msaada wetu kwa ubaya na mitego yote ya shetani, ili Mungu akuamuru, tunakuomba na tunakusihi, nawe mkubwa wa jeshi la Mungu, tupa katika jehenama, kwa nguvu ya Mungu, shetani na pepo mengine mabaya yanayozunguka duniani kwa kupoteza roho za watu. **Amen**.

- Mtakatifu Mikaeli-Mkuu, utuombee (X3)

**MWENDO WA MKUTANO WA WALAIKI WA MISIONARI NA REHEMA YA MUNGU**

1. Wimbo wa mwanzo
2. Alama ya Msalaba
3. Nia ya sala ao ya mkutano
4. Shapule ya Rehema ya Mungu ao Shapule ya kawaida
5. Kualika Roho Mtakatifu
6. Kusoma Neno la Mungu - mafasirio
7. Maombi
8. Wimbo wa Sifa kwa Heshima ya Rehema ya Mungu
9. Matoleo
10. Kuwapokea wageni
11. Habari mbalimbali na mipango ya gundi
12. Sala ya kujitolea kwa Yesu Mwenyi Huruma
13. Wimbo wa mwisho

**KANUNI ZA MSINJI ZA MAISHA YA MKRISTU**

**Amri za Mungu**

1. Umuabudu Mungu mmoja tu, ukampende kwa moyo wako wote
2. Usitaje bure jina la Mungu
3. Uifanye takatifu siku ya Mungu
4. Uwaheshimu Baba yako na Mama yako
5. Usiuwe
6. Usizini
7. Usiibe
8. Usishudu uwongo wala kusema uwongo
9. Usitamani mtu asiye ndowa yako
10. Usitamani kuiba mali za watu

**Sakramenta saba za Eklezya**

1. Ukaristia
2. Usabitisho
3. Ukaristia
4. Kitubio
5. Mpako wa wagonjwa
6. Daraja ya Upadirisho
7. Ndoa

**Amri mbili za mapendo**

1. Umpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote
2. Umpende jirani kama unavyojipenda mwenyewe.

**Sifa za heri**

- Heri walio maskini moyoni kwani Ufalme wa mbinu ni wao
- Heri walio wapole, kwani hao watarisi inchi
- Heri wenyi uchungu, kwani hao watatulizwa
- Heri wenyi njaa na kiu cha kupata utakatifu, kwani hao watashoba
- Heri wenyi huruma, kwani hao watahurumiwa
- Heri wenyi moyo safi, kwani hao watamwona Mungu
- Heri wenyi kuletaa amani, kwani hao wataitwa waana wa Mungu
- Heri wenyi kuzulumiwa kwa ajili ya unyofu, kwai Ufalme wa mbingu ni wao
- Heri yeni nyinyi kama watu wanawatukana na kuwazulumu na kuwachongea uwongo kwa ajili yangu mimi na kwa ajili ya enjili. Furani na shangilieni kwani tuzo yenu ni kubwa Mbingui.

**Vipaji saba za roho Mtakatifu**

1. Hekima
2. Akili
3. Shauri
4. Nguvu
5. Elimu
6. Ibada
7. Uchaji wa Mungu.

**Matunda kumi na mbili ya Roho Mtakatifu**

1. Mapendo
2. Furaha
3. Amani
4. Uvumilivu
5. Ustamilivu
6. Uaminifu
7. Wema
8. Upole
9. Rehema
10. Unyenyekevu
11. Uafi wa roho (utawa)
12. Usafi.

**Amri za Eklezya**

1. Uifanye takatifu siku ya Mungu ; nendo ku misa na uache kazi
2. Usikose kuungama zambi zako kila mwaka

3. Usikose kukomonika vema wakati wa Pasaka
4. Ujikatalie kula nyama na uheshimu mfungo siku zinazoamriwa na Eklezya
5. Usikose kusaidia Eklezya na mali yako.

**Matendo saba ya Huruma ya Kiroho**

1. Kuwaonya wenyi zambi
2. Kufundisha watu wasiojua
3. Kushauria wenyi masito
4. Kuwatuliza wenyi uchungu
5. Kuwavumilia wenyi uchokozi
6. Kusamehe kwepesi
7. Kuwaombea wazima na wafu.

**Matendo saba ya Huruma ya Kimwili**

1. Kuwagawia wenyi njaa chakula
2. Kuwapa wenyi kiu kinywaji
3. Kuwavika walio uchi mavazi
4. Kuwapangisha wasio na makao
5. Kuwatembelea wafungwa gerezani
6. Kuwatembelea wagonjwa
7. Kuwazika wafu.

**Zambi kubwa saba**

1. Majivuno
2. Uchoyo
3. Wivu
4. Hasira
5. Unajisi (ujusi)
6. Ulafi
7. Uvivu

**Mambo ya mwisho wa wanadamu**

1. Kifo
2. Hukumu
3. Jehanama
4. Mbingu.